

**TAASISI YA UTAFITI NA UTETEZI WA HAKI ZA ARDHI
(HAKIARDHI)**

**UCHAMBUZI WA MASUALA YA ARDHI YALIYORIPOTIWA NA
VYOMBO VYA HABARI KWA MWAKA 2011**

Umeandaliwa na;

Cathbert Tomitho

YALIYOMO

1. UTANGULIZI	3
2. MASUALA YALIYOIBUKA.....	3
I. UWEKEZAJI KATIKA ARDHI	3
II. MIGOGORO YA ARDHI NCHINI	10
a. Migogoro baina ya wakulima na wafugaji	11
b. Migogoro baina ya wananchi na wawekezaji	12
c. Migogoro ya mipaka baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi	13
d. Ufanyaji kazi wa vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi	14
e. Nafasi ya wanasiasa na watendaji wa serikali katika migogoro ya ardhi	16
f. Uelewa duni wa sheria za masuala ya ardhi	18
g. Madhara ya migogoro ya ardhi	19
III. UVAMIZI WA ARDHI	20
IV. BOMOABOMO, UHAMISHWAJI KATIKA ARDHI NA FIDIA YA ARDHI KWA WANANCHI.....	23
V. UWEKEZAJI KWENYE SEKTA YA MADINI	26
VI. MATUMIZI YA ARDHI KWA KILIMO	29
VII. UFUGAJI NA WAFUGAJI	31
VIII. MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIA YA NCHI.....	32
IX. UPIMAJI NA UMILIKI WA ARDHI	34
X. MCHAKATO WA KATIBA MPYA NA NAFASI YA ARDHI	35
XI. SUALA LA ARDHI KATIKA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI.....	36
XII. MRADI WA MJI MPYA KIGAMBONI.....	36
XIII. UWEKEZAJI KATIKA ARDHI YA VIJJI KWA UZALISHAJI WA NISHATI UOTO.....	37
3. HITIMISHO.....	38

1. UTANGULIZI

Ardhi ni rasilimali muhimu kwa maisha ya kila binadamu kwa njia moja ama nyingine. Umuhimu wa ardhi unaonekana kwa kutazama mchango wake katika maisha ya kila siku kwa mtu mmoja mmoja, makundi ya watu, serikali, makampuni na sekta nyingine. Kwa nchi za dunia ya tatu kama Tanzania ardhi ni rasilimali ya kipekee katika kuendesha maisha ya watu wake. Inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 75 ya watanzania wote wanategemea ardhi kuendeshea maisha yao ya kila siku. Utegemezi huu wa asilimia 75 umejikita katika wale waliojiingiza katika kilimo, ufugaji na kazi nyingine zinazotegemea ardhi ukiachilia mbali wale wanaofanya kazi katika makampuni na taasisi mbalimbali za umma na binafsi.

Ardhi nchini Tanzania ina historia ndefu katika nyakati mbalimbali za kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na wakati wa uhuru hadi mwaka 2011 tulipoadhimisha miaka 50 ya uhuru. Katika nyakati zote hizi kumekuwepo masuala na matukio mbalimbali yaliyotokea na yanayozidi kuibuka ikiwa ni pamoja na masuala ya uwekezaji katika ardhi, migogoro ya ardhi baina ya makundi yanayotumia ardhi, mabadiliko ya tabia ya nchi na mazingira, masuala ya kilimo na mikakati mbalimbali ya sekta hii kama vile Kilimo Kwanza, uvamizi wa ardhi katika maeneo mbalimbali nchini, kukua na kupanuka kwa miji na majiji, masuala ya fidia kwa miradi ya umma kama vile ujenzi wa barabara na upanuzi wa miji kama vile Kigamboni.

Kutokana na masuala haya kuibuka mara kwa mara wakati mwingine yakiwa na faida kwa jamii na wakati mwingine yakiwa na madhara kwa jamii. Vyombo vya habari vimekuwa vikiripoti habari hizi kila siku kutoka maeneo mbalimbali nchini. Kwa mwaka 2011 habari nyingi za masuala ya ardhi ziliripotiwa kwa kiwango kikubwa katika maeneo mbalimbali na kwa sura tofauti tofauti. Ufuatao ni uchambuzi wa masuala haya yaliyoibuka kwa mwaka mzima wa 2011 na kuripotiwa kwenye magazeti mbalimbali nchini.

2. MASUALA YALIYOIBUKA

I. UWEKEZAJI KATIKA ARDHI

Uwekezaji ni jitihada za kuifanya maliasili ya nchi kuwa katika rasilimali kwa kutumia nyenzo kama mtaji, teknolojia na nguvu kazi. Kinachotokana na uzalishaji hurejeshwa katika kuimarisha miundombinu, mitaji, teknolojia na rasilimali (watu, fedha, malighafi) ili faida iweze kupatikana na pale inapopatikana faida ndipo matunda ya maendeleo huonekana kwavile faida hiyo hutumika kukidhi mahitaji ya muhimu na ya ziada kwa mwenye mali au aliyewekeza. Katika nchi za dunia ya tatu Tanzania ikiwa mojawapo uwekezaji umekuwa ukifanywa na kundi dogo la wananchi wa ndani na nje ya nchi.

Eneo muhimu la uwekezaji nchini Tanzania ni ardhi hasa katika kilimo na ufugaji, madini pamoja na utalii.

Kwa mwaka 2011 taarifa za uwekezaji zilijikita zaidi katika ardhi ya vijiji kwa ajili ya kilimo kwanza na mazao ya nishati uoto. Habari kubwa zilizoripotiwa ni pamoja wawekezaji wakubwa kukumbwa na kashfa ya upendeleo na kuchukua maeneo makubwa ya ardhi na kuingia katika mikataba feki na inayowanufaisha wao zaidi kuliko wananchi waliotoa ardhi zao kwa ajili ya uwekezaji. Mikataba ya kupata ardhi imekuwa ya siri zaidi isiyowashirikisha wanavijiji wa maeneo husika wakati wa kusaini na hata baada ya kusaini imekuwa haipatikani kwenye ofisi za vijiji. Mara nyingi mikataba hii imekuwa na ahadi zisizotekelezeka kama vile ahadi za ujenzi wa madarasa ya shule, urekebishaji wa barabara, ajira kwa vijana na wanawake, ushirikiano wa teknolojia inayotumika na wawekezaji kwenye uzalishaji wa mazao na kwenye viwanda. Pamoja na mambo mengine wawekezaji hawa wanalalamikiwa kwa kushindwa kutunza mazingira katika maeneo wanayochukua kwa uwekezaji kama vile kwenye migodi mfano mgodi wa North Mara wilayani Tarime na kwenye mashamba ya nishati uoto (jatropha) wilayani Kilwa¹.

Mfano huko wilayani Mbarali wakazi wa kijiji cha Nsonyanga waliilalamikia serikali kwa kuwafumbia macho wawekezaji wanaotumia mikataba bandia kwa lengo la kuwalaghai. Madai ya wananchi hao yalitokana kampuni ya Quarry Associates Limited iliyowekeza katika uchimbaji kokoto kwa miaka mitano kijijini hapo kushindwa kutekeleza ahadi zake ikiwepo ya kuwalipa wakazi wa eneo hilo Tsh. 15 milioni kila mwaka pamoja na kuboresha huduma za afya, maji na kutunza mazingira².

Suala la mikataba mibovu lilionekana pia kwenye utekelezaji wa yaliyoainishwa kutekelezwa kwa jamii lakini pia kwa wawekezaji wenyewe kutumia maeneo waliyoyaomba kwa matumizi yaliyokusudiwa. Wilayani Rufiji katika kijiji cha Nyamwage wananchi walikilalamikia Kituo cha Uwekezaji TIC kwa kuwapelekea mwekezaji ambaye ameshindwa kuendeleza hekta 5,000 za ardhi alizopewa miaka sita iliyopita. Wananchi walilalamika kuwa mwekezaji huyo raia wa Uturuki ametelekeza eneo hilo ambalo limekuwa kero kwa wanavijiji kutokana na kuwa pori kubwa linalotisha. Pia limekuwa kikwazo kwa maendeleo ya wananchi kutokana na kushindwa kutumika na wanavijiji wasiokuwa na maeneo ya kutosha kwa kilimo na makazi³.

Utekelezaji wa mashamba pia ulionekana katika maeneo mengine ya nchi kama vile wilayani Kilwa ambapo kampuni ya Bioshape imetelekeza shamba ililochukua kwajili ya

¹ The Citizen la Februari 2, 2011

² Nipashe Agosti 18, 2011

³ Mwananchi Mei 17, 2011

kilimo cha nishati mbadala lenye ukubwa wa hekta 34,000. Pia kampuni ya Sunbiofuel wilayani Kisarawe ambayo imekuwa inaendeleza kwa kusuasua eneo la hekta 8,000 kiasi cha kuwaacha pasipo kujua hatima yao wafanyakazi takribani 300 waliokuwa awali wameajiriwa katika mashamba hayo⁴. Hali ya utekelezaji wa mashamba yanayomilikiwa na wawekezaji ulijitokeza pia mkoani Lindi ambako wananchi zaidi ya 200 katika kijiji cha Mkwaya wakiwa na silaha za jadi walivamia mashamba ya kampuni ya Indo African Estate na kugawana. Wananchi hao walitoa sababu za kuvamia mashamba hayo kuwa ni mwekezaji huyo kushindwa kuendeleza ardhi hiyo, *“Mwekezaji huyu anamiliki kisheria eneo hili lakini haonyeshi dhamira ya kuliendeleza hasa ukizingatia kuwa ni muda mrefu sana tangu alipopewa eneo hilo, huku sisi tukiangaika kupata maeneo ya kilimo wakati kuna eneo lililo wazi⁵”* walisema wananchi hao walipotakiwa kueleza sababu za kuvamia eneo hilo. Wilayani Mkuranga, madiwani wa halmshauri hiyo nao walichukua maamuzi magumu ya kumtimua mwekezaji Shadhil anayemiliki kampuni ya Green Belt Oil kutokana na dhamira yake ya kuwekeza kugubikwa na ubabaishaji mkubwa⁶.

Kutokana na kuongezeka matukio mbalimbali yanayosababishwa na baadhi ya wawekezaji hasa kwenye ardhi ya vijiji. Wananchi wengi wameanza kutafuta uelewa wa haki na wajibu wao katika ardhi inayowazunguka. Mfano mzuri ni katika wilaya ya Rufiji ambako wananchi wa vijiji vya Nyama, Lungungu, Nyamatanga na Mbawa wilayani Rufiji walimtaka aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani Hajati Amina Mrisho kumuamuru mwekezaji wa kampuni ya kilimo cha michikichi ya African Green Oil Ago kurejesha ardhi yao zaidi ya hekta 2,500 kwa madai ya kuendesha mradi kinyume na makubaliano yao pamoja na vitendo vya kinyanyasaji kwa watumishi. Mwekezaji huyo aliwaahidi wananchi kuwa angeboresha huduma za afya, elimu na maji ambavyo vyote havijatekelezwa huku mradi huo ukiingia mwaka wa tatu. Jambo la kushangaza zaidi kutoka kwa mwekezaji huyo ni kulalamika kuwa mtaji uliowekezwa wa bilioni 2 hauendelei vizuri kutokana na eneo hilo kuwa bovu kwa kilimo cha michikichi na kupeleka ombi la kutaka hekari 3,000 zaidi kwenye sehemu ya mto Rufiji jambo ambalo lilipingwa kwa nguvu zote na wananchi wa maeneo hayo⁷.

Suala la ushirikishwaji duni wa wananchi kwenye maamuzi yanayohusiana na masuala ya ardhi lilijitokeza sana kwa mwaka 2011. Huko wilayani Rungwe wakulima wa chai walipinga mashamba yao kubinafsishwa kwa kampuni ya WATCO inayomiliki kiwanda cha Katumba. Malalamiko ya wananchi yalitokana na kiwanda hicho ambacho hapo

⁴ Mwananchi Mei 17,2011

⁵ Mwananchi September 24, 2011

⁶ Tanzania Daima Agosti 14, 2011

⁷ Tanzania Daima Januari 10, 2011

awali kilikuwa kinamilikiwa na serikali kubinafsishwa kwa WATCO iliyochukua jumla ya hisa za asilimia 70 wakati Umoja wa Wakulima wadogo wa chai Rungwe (RSTGA) ukimiliki hisa asilimia 30. Madai ya wananchi hawa yalitokana na taarifa kuwa ardhi yote inayotumika kwa kilimo cha chai imebinafsishwa kwa kampuni hiyo na wakulima watabaki kuwa wakodishaji tu kwenye ardhi hiyo. Suala kubwa lililoonekana katika sakata hilo ni kukosekana kwa ushiriki wa wakulima wakati wa mchakato wa kubinafsisha mashamba hayo. Uelewa wa wakulima katika masuala ya hisa na mikataba ulitakiwa kuzingatiwa kabla ya serikali kuchukua jukumu la kubinafsisha mashamba husika⁸.

Kuendelea kukosekana kwa ushirikishwaji madhubuti wa wananchi kwenye maamuzi kulipelekea wananchi wengi kuibuka na kudai haki zao pale walipogundua kuwa walidhulumiwa katika maamuzi ya awali. Uongozi wa Mkoa wa Mbeya ulilazimika kuwapa wananchi wa wilaya ya Mbarali shamba jipya lenye ukubwa wa hekari 6,000 katika jitihada za kumaliza mgogoro baina ya wanakijiji hao na mwekezaji kwenye shamba la Mbarali Estate. Serikali ilisema haiwezi kulirudisha shamba la awali kwa wananchi kutokana na ukweli kuwa shamba hilo tayari lilishauzwa kwa mwekezaji⁹. Maamuzi haya ya kukurupuka katika ngazi za juu za serikali ni ya kusikitisha na kutia mashaka kutokana na ukweli kuwa yana athari kubwa sana katika kuboresha maisha ya wananchi kutokana na kuonekana dhahiri kuwa yana upendeleo kwa watu wachache wa tabaka la juu.

Katika mtazamo wa jumla uwekezaji mbovu kwenye ardhi nchini Tanzania una sababu nyingi kubwa ikiwa ni utendaji mbovu wa viongozi nchini kuanzia ngazi ya kijiji mpaka taifa. Mfano huko Mwanza aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Abbas Kandoro alipiga marufuku viongozi wote wa serikali za vijiji mkoani humo kuuza ardhi kwa wawekezaji pasipo kuwashirikisha wananchi wote. Agizo hilo la Mkuu wa Mkoa lilitokana na kushamiri kwa malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa maeneo mengi yamekuwa yanagawiwa kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa usiri mkubwa sana. Kwa mujibu wa sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya 1999 ni Mkutano Mkuu wa Kijiji ndicho chombo pekee chenye mamlaka ya kupitisha maamuzi ya kugawa ardhi ya kijiji. Lakini hili limekuwa likitendwa kinyume na watendaji wa vijiji mbalimbali nchini.¹⁰

Pamoja na sheria ya uwekezaji kuainisha viwango vya mitaji wanayotakiwa kuwa navyo wawekezaji kabla ya kuanza kuwekeza. Huko mkoani Kagera wawekezaji katika ranchi ya Misenyi wameiomba serikali iwe na subira ili waweze kuendeleza maeneo

⁸ Nipashe Januari 14, 2011

⁹ Mwananchi Machi 13, 2011

¹⁰ Majira Januari 1, 2011

waliyokabidhiwa. Wawekezaji hao wamekuwa wakitoa hoja kuwa kuna masuala ya kitaalamu yanayowakwamisha ambayo pindi watakapoyarekebisha uzalishaji utaanza mara moja¹¹ lakini ni muda mrefu sasa mradi huo umeshindikana kuanza. Wakati hali hiyo ikijitokeza huko Misenyi, wilayani Kilombero wawekezaji wa Kilombero Plantations Limited (KPL) walikuwa kwenye mchakato wa kuanza kujenga nyumba 60 zenye thamani ya Tsh. 180 milioni kwa wananchi wanaozunguka shamba hilo ambapo kila nyumba itagharimu Tsh. 3 milioni. Ujengaji wa nyumba hizi unaendana sambamba na ulipwaji wa fidia kwa wananchi waliokuwa wanatumia mashamba ya kampuni ambao walilazimika kuondoka na kuipa nafasi kampuni kupanua kilimo kikubwa cha mpunga inachokiendesha¹². Pamoja na utekelezaji wa ahadi za kampuni hii bado kuna malalamiko kuwa unyunyiziwaji wa dawa kwenye kilimo kinachoendeshwa na kampuni hiyo umekuwa unaathiri mashamba ya jirani yanayomilikiwa na wanavijiji.

Katika upande mwingine uwekezaji katika ardhi nchini umekuwa chanzo cha migogoro mingi sana ambayo inasababishwa na kukosekana kwa makubaliano wakati wa kuchukua ardhi kutoka kwa wananchi. Mgogoro baina ya wananchi wa Ngorongoro na kampuni ya uwekezaji ya uwindaji ya Ortello Bussiness Company (OBC) inayomiliki zaidi ya kilomita za mraba 4,000 za eneo la Loliondo¹³ ni mfano mzuri. Mgogoro huu ambao umedumu kwa muda mrefu sasa umepelekea majanga mengi kwa wananchi wa kawaida wa maeneo ya Loliondo kama vile upotevu wa mifugo yao, kufukuzwa mara kwa mara kwenye maeneo wanayoishi na kufugia hali inayopelekea kuharibu maisha yao ya kiuchumi na kijamii. Mgogoro katika eneo la Loliondo umeendelea kuripotwa kwa kiasi kikubwa kwa mwaka wa 2011 kutokana na kuchukua sura mpya kila wakati.

Katika hali inayoonyesha kushamiri kwa migogoro inayotokana na uwekezaji, wananchi wa kitongoji cha Kinyenzi wilayani Mvomero walitangaza hali ya hatari dhidi ya mwekezaji wa kigeni anayedaiwa kupora ardhi ya wananchi wa eneo hilo. Mwekezaji huyo alidaiwa kuzungushia uzio katika mashamba yao zikiwemo nyumba zao na shule ya kitongoji hicho. Mgogoro huo ambao hadi mwezi Septemba mwaka 2011 ulikuwa umedumu kwa kipindi cha miezi mitatu¹⁴. Hali hii inaonyesha ni kwa jinsi gani ambavyo kukosekana kwa mipango bora ya matumizi ya ardhi vijijini kunavyosababisha uvunjifu wa amani kutokana na wajanja wachache kwa majina ya wawekezaji wanavyojinyakulia mashamba ya wananchi kwa jinsi wanavyopenda wao. Ni katika wilaya hiyo hiyo ya Mvomero wakulima wa miwa walimuomba Mbunge wa jimbo hilo Bwana Amos Makalla kuhakisha kuwa wanalipwa fedha zao na kiwanda cha sukari cha Mtibwa baada ya kukiuzia miwa katika msimu wa mwaka jana, *“Tumekuwa na mgogoro na kiwanda cha*

¹¹ Nipashe Agosti 21, 2011

¹² Majira Agosti 11, 2011

¹³ The Citizen September 19, 2011

¹⁴ Nipashe Septemba 10, 2011

Mtibwa kwa kushindwa kuwalipa kwa wakati madai ya fedha za mauzo ya miwa ya wakulima hali inayopelekea wananchi kurudi nyuma kimaendeleo na hivyo kushindwa kuchangia maendeleo ya kijiji chetu” alisema Mtendaji wa kijiji Mtibwa Bwana Simon Myogo¹⁵.

Wimbi la ongezeko la migogoro ya ardhi nchini baina ya wawekezaji na wananchi lilipelekea aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha Bwana Isidori Shirima kuwataka wawekezaji mkoani humo kuheshimu mamlaka za serikali za vijiji ili kuepusha mahusiano mabaya baina yao na wananchi. Mkuu huyo wa Mkoa aliwataka wawekezaji kufahamu kuwa wenye uwezo wa kuwapa ardhi ni serikali za vijiji na siyo uongozi wa juu wa serikali kama wengi wanavyodhani. *“Wawekezaji wakitambua kuwa serikali za vijiji ni mamlaka halali na kushirikiana nazo ipasavyo amani itadumu”* alisema Mkuu huyo wa Mkoa¹⁶. Wakati Mkuu huyo wa Mkoa akitoa ushauri huo, uko wilayani Misenyi mkoa wa Kagera baadhi ya familia zilitoa malalamiko kuwa Mkuu wa wilaya hiyo Kanali Issa Njiku alitoa amri ya kuchomwa kwa nyumba 36 ambazo zilikuwa kwenye eneo linalodaiwa kuwa la mwekezaji. Wananchi hao wa kitongoji cha Kazizi, kijiji cha Bubare walilalamikia hatua hiyo ya Mkuu wa wilaya kuwa ni ya upendeleo kutokana na kutosikiliza malalamiko yao na kutoa hukumu kutokana na maelezo ya mwekezaji pekee¹⁷.

Kama ilivyo ada ya migogoro sehemu yoyote kuwa hatima yake ni madhara hasi yanayosababisha uhasama, vifo na uharibifu wa mali. Kampuni ya Grumeti Reserve inayomiliki vitalu vya uwindaji katika pori la akiba la Ikorongo na Grumeti Serengeti ilidaiwa kuingia katika makubaliano ya kulipa ng’ombe 15 kama fidia kwa familia ya Richard Disman (28) aliyeuawa kwa risasi na askari wa kampuni hiyo tarehe 22 Agosti 2011 katika mazingira ya kutatanisha¹⁸. Haya ni baadhi tu ya madhara yanayosababishwa na migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini.

Wakati masuala hayo yakiibuka katika uwekezaji kwenye ardhi mengi yake yakionekana kuwa yasiyokuwa na manufaa kwa wananchi. Kituo cha Uwekezaji Nchini (TIC) kimesema kuwa juhudi za serikali za kujenga mazingira bora ya uwekezaji zimezaa matunda baada ya kuongezeka kwa thamani ya mitaji iliyowekezwa nchini hadi dola za Marekani milioni 700 mwaka 2010 kulinganisha na dola milioni 645 kwa mwaka 2009. Takwimu hizo zilitokana na taarifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD) ambayo inaonyesha kuwa Tanzania imechukua nafasi ya pili

¹⁵ Nipashe Januari 8, 2011

¹⁶ Nipashe Mei, 2011

¹⁷ Mwananchi Julai 27, 2011

¹⁸ Mwananchi Septemba 21, 2011

katika eneo la jumuiya ya Afrika Mashariki na kati ikiongozwa na Uganda¹⁹. Kauli ya TIC kwa kiasi kikubwa inapingana na uhalisia katika maeneo mengi ambayo wawekezaji wamewekeza hasa hasa katika ardhi. Bado kwa kiwango kikubwa wawekezaji hawa wameshindwa kuonyesha kwa dhati kuwa dhamira yao ni kuwekeza katika kukuza uchumi wa nchi. Inawezekana kwa tafsiri hiyo ya kuongezeka kwa mitaji kwa wawekezaji kukawa hakuonekani katika uhalisia ambao wananchi pamoja viongozi waliutegemea kuwa mchango wa uwekezaji katika uchumi wa nchi na watu wake.

Wakati Asasi za Kiraia nchini na vyombo vya habari vikiripoti masuala ya uwekezaji nchini ambayo kwa kiwango kikubwa yamekuwa si ya kupendeza, viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya taifa hadi vijiji wameendelea kuvutia wawekezaji kwenye ardhi maeneo mbalimbali nchini. Kwa mfano kampuni ya Agrisol Energy Tanzania ambayo imeonyesha nia ya kuwekeza katika mkoa ya Rukwa, Kigoma na Katavi imeendelea na mchakato wake na Halmashauri ya wilaya ya Mpanda kuhusu matumizi ya ardhi katika maeneo ya Katumba na Mishamo wakati kukiwa na mitizamo tofauti kuhusiana na uwekezaji huo kuwa hautokuwa na manufaa ya kutosha kwa umma wa Watanzania. Wakati baadhi ya wananchi, watendaji wa vijiji na madiwani wakipinga makubaliano ya awali na mwekezaji huyo ya kukodishiwa mashamba hayo kwa miaka 99 kwa malipo ya Tsh. 200/= kama kodi ya ardhi kwa hekari moja wakati Halmashauri ikipata Tsh. 500/= kwa hekari pasipo kuainishwa wazi ni katika kipindi gani malipo hayo yatakuwa yanalipwa aidha kila siku, mwezi au mwaka. Suala lingine linalotia shaka ni usuluhishi wa migogoro ambao pale muafaka utakapokosekana hapa nchini basi utapelekwa kusikilizwa kwenye chemba ya biashara ya kimataifa jijini London, Uingereza. Pamoja na kasoro hizi za awali lakini bado viongozi wa Halmashauri za wilaya na wale wa serikali kuu wameendelea kuupigia debe uwekezaji huo kuwa utaongeza ajira na akiba ya chakula nchini²⁰.

Suala uwekezaji kwenye mashamba ya Mishamo na Katumba na maeneo mengine ya nchi yalionekana kuligusa hata Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye vikao vya bajeti. Kambi ya Upinzani iliitaka serikali kuachana na wazo la kutoa hati ya umiliki wa zaidi ya hekari 327,755 wilayani Mpanda kwa kampuni ya uwekezaji kutoka Marekani ya Agrisol Energy. Kambi ya Upinzani ilitoa wazo kwa serikali kutafuta wawekezaji zaidi katika miundombinu ambayo ikiboreka hata wananchi wa kawaida watashiriki katika uwekezaji na kufaidika na rasilimali zao tofauti na leo ambapo wananchi wamegeuka kuwa manamba na vibarua kwenye mashamba ya wawekezaji wakubwa kwa malipo kidogo²¹.

¹⁹ Majira Julai 29,2011

²⁰ Nipashe Julai 31, 2011

²¹ The Citizen Julai 27, 2011

Katika mtazamo mwingine kwenye masuala ya uwekezaji Mhadhiri wa masuala ya kilimo kwenye Chuo Kikuu cha Sokoine Dr. Damian Gabagambi aliiasa serikali kuwa makini na suala la ardhi kwa kuacha kuwamilikisha wageni kwa mgongo wa uwekezaji mkubwa katika kilimo kwa fikra kwamba nchi ina ardhi kubwa na ya kutosha. Aliongeza kuwa mtindo wa sasa kupitia kwenye kauli ya kilimo kwanza unaoruhusu kila mwenye fedha kujichukulia ardhi kubwa awezavyo na kulima chochote anachotaka mwisho wa siku utaleta matatizo ambayo yanaweza kuitumbukiza nchi kwenye machafuko. Alipendekeza kuwa jambo la muhimu ni kwa serikali kupima ardhi yote na kisha kuitenga ili kila sehemu iwe na matumizi yake maalumu kama kuendesha kilimo cha mazao ya biashara, chakula, viwanda, ujenzi na shughuli nyinginezo. Pia alishauri kuwa wawekezaji wawepo lakini waingie ubia na wakulima au wakodishe ardhi na kulipa kodi inayostahili katika mamlaka husika²². Ni katika mtazamo huo huo ambapo viongozi wa dini zote nchini walitoa tamako kuhusu mabadiliko ya hali ya tabia ya nchi wakionya kuwa uwekezaji na ubinafsishaji visiwe vigezo vya kupora rasilimali za wazawa na kuwapa wageni²³.

Kwa tathimini ya haraka kuhusiana na hali ya uwekezaji katika ardhi hali halisi inaonyesha kuwa bado kuna safari ndefu sana katika kupata mafanikio kupitia uwekezaji. Kumekuwa na malalamiko na migogoro mingi kutoka kwa wananchi na wakati mwingine viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya serikali za mitaa hadi serikali kuu kuhusiana na vitendo vya wawekezaji vikiwemo kutelekeza maeneo na kusababisha migogoro baina yao na wananchi. Suala la muhimu linalohitajika ni kwa serikali kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinafuatwa katika kutekeleza sera ya uwekezaji. Hii itawezekana tu kwa serikali kuwabana wawekezaji na viongozi wote wa serikali wanaokiuka sheria za nchi katika utoaji wa hatimiliki za ardhi. Pia suala la ushiriki wa wananchi ni la kuzingatiwa sana hasa ikizingatiwa kuwa wao ndio waathirika wa kwanza wa matatizo yanayosababishwa na uwekezaji.

II. MIGOGORO YA ARDHI NCHINI

Migogoro ya ardhi nchini imekuwa ikiibuka kila nyakati baina ya makundi mbalimbali ya watumiaji wa ardhi. Makundi haya ni pamoja na wakulima na wafugaji, kijiji na kijiji, wawekezaji na wananchi kwenye migodi ya madini na mashamba makubwa, pamoja na mamlaka za hifadhi na wananchi. Vyanzo vya migogoro hii ni pamoja utekelezaji usioridhisha wa sheria za ardhi ikiwa ni pamoja na sheria za ardhi za mwaka 1999, sheria mpango bora wa matumizi ya ardhi ya mwaka 2007 na sheria nyinginezo za

²² Nipashe Julai 30, 2011

²³ Mwananchi Septemba 22, 2011

mipango miji na sheria ya uwekezaji. Pia kuna suala zima la mabadiliko ya tabia ya nchi ambayo yamepelekea uhaba wa mvua na maji hali inayopelekea kupungua maeneo yenye rutuba. Kwa mwaka 2011 masuala mengi ya migogoro ya ardhi yalijitokeza na kuripotiwa kwa wingi katika vyombo vya habari kama inavyoonekana.

a. Migogoro baina ya wakulima na wafugaji

Mapigano makali yaliibuka baina ya wakulima na wafugaji katika kijiji cha Kongwa, tarafa ya Mvuha, mkoani Morogoro. Katika mapambano hayo nyumba saba za wafugaji ziliteketezwa kwa moto. Chanzo cha mapambano hayo ni wafugaji watatu kuingiza mifugo yao katika mashamba ya wakulima tarehe 28 Agosti 2011²⁴. Katika mgogoro mwingine baina ya haya makundi mawili, wafugaji na wakulima wa kijiji cha Kivinja “A”, kata ya Mwambao walipigana baada mkulima mmoja kumtuhumu mfugaji kuchoma moto shamba lake kwa lengo la kuandaa eneo hilo kwa malisho. Katika mapambano hayo ambayo watu wanne walijeruhiwa kwa mapanga na silaha nyingine za jadi, ikiwemo mkulima kumkata mfugaji kwa mapanga kichwani. Hali hiyo ilipelekea wafugaji kujiunga katika makundi na kwenda kulipiza kisasi kwenye familia za wakulima ambapo walimjeruhi mtoto wa mkulima²⁵.

Migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji ilizidi kusababisha madhara kwa jamii, mfano huko mkoani Morogoro, wilayani Kilombero katika kata ya Chissano tarafa ya Mlimba. Watu wanaosadikiwa kuwa ni wafugaji wa jamii ya Kisukuma walimuuu kwa kumnyweshwa sumu ya kuulia magugu Afisa Mtendaji Bw. Faustine Kaduvaga tarehe 23 Julai 2011 majira ya asubuhi wakati Mtendaji huyo akielekea kwenye kituo chake cha kazi. Hali hii ya kusikitisha ilisababishwa na mgogoro uliodumu kwa muda mrefu baina ya wakulima na wafugaji katika eneo hilo na msimamo wa Mtendaji huyo katika kuhakikisha kuwa hatoi upendeleo kwa kundi lolote²⁶. Huko mkoani Manyara wilaya ya Kiteto wafugaji wenye asili ya Kimaasai wametuhumiwa kuwa chanzo cha migogoro ya ardhi kwa kuchunga mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima nyakati za usiku. Kwa mujibu wa Mtendaji wa Kijiji cha Ndaleta Bi. Fatuma Ngao, wafugaji wamekumbwa na tatizo kubwa la malisho kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi hali inayopelekea mifugo yao mingi kupoteza maisha nyakati za kiangazi²⁷.

Huko wilayani Ngorongoro, eneo la Loliondo zaidi ya vijiji 13 viliingia katika migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji jambo lililopelekea kudorora kwa maendeleo ya wananchi. Pamoja na migogoro hii kudumu kwa muda mrefu sasa lakini bado utatuaji

²⁴ Mwananchi Septemba 5, 2011

²⁵ Mwananchi Septemba 24, 2011

²⁶ Tanzania Daima Julai 23, 2011

²⁷ Majira Septemba 9, 2011

wake haujawa makini kutokana na serikali kutotilia mkazo mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo hayo. Pia tatizo la uelewa mdogo wa sheria za ardhi na nafasi ya wananchi katika utatuzi wa migogoro ya ardhi umekuwa ndio chanzo kikubwa katika kuendelea kukua kwa migogoro hiyo. Halikadhalika kukosekana kwa mipaka madhubuti baina ya vijiji kumepelekea kuongezeka kwa migogoro hiyo kila mara²⁸. Wilayani Bagamoyo mgogoro uliodumu kwa muda mrefu baina ya wakulima na wafugaji katika vijiji viwili tofauti vya Pingo na Chamakweza ulielekea kufikia ukingoni baada ya serikali za vijiji vyote viwili kukubaliana kupambana na wale wote ambao wanatuhumiwa kuchukua maeneo ya wakulima na wafugaji kinyume cha sheria. Kukubaliana kwa vijiji hivi kutatua mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu ni suala muhimu sana hasa ikizingatiwa kuwa madhara yake ni makubwa sana katika maeneo ya vijijini²⁹.

b. Migogoro baina ya wananchi na wawekezaji

Migogoro baina ya wananchi na wawekezaji nchini ilizidi kuongezeka kila mara katika maeneo ambayo wawekezaji wamewekeza. Mfano wa mgogoro mkubwa uliofukuta katika bonde la Kiru lenye ukubwa wa hekari 96,000 zinazofaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali wilayani Babati mkoani Manyara ambao umekuwa na historia ndefu yenye machungu kwa wananchi na wawekezaji. Matatizo hayo yamekuwa yakichangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo ongezeko la watu na mabadiliko ya hali ya hewa katika bonde hilo ambalo limepelekea kuwepo na uhitaji mkubwa wa ardhi hasa yenye rutuba na inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Mgogoro katika bonde hili kwa miaka ya karibuni ulisababisha madhara mengi yakiwemo umwagikaji wa damu, kuchomwa kwa nyumba na mali nyingine, kutelekezwa kwa familia kutokana na baadhi ya wananchi wa eneo hilo kukumbwa na hofu ya kukamatwa na vyombo vya dola kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya uharibifu wa mali za wawekezaji³⁰. Kwa mujibu wa maelezo ya wananchi na watafiti mbalimbali ikiwa ni pamoja na waandishi wa habari mgogoro huu unakuzwa na vitendo vya baadhi ya viongozi wa serikali ngazi ya mkoa na wilaya kuwalinda wawekezaji pasipo kuwasikiliza wananchi waliozunguka mashamba hayo.

Uwekezaji katika nishati uoto pia ulitajwa kuwa sehemu ya chanzo cha migogoro baina ya wawekezaji na wananchi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa kwenye maeneo ambayo uwekezaji huu umefanyika wananchi wamezuiwa kuendelea kutumia vyanzo vya maji walivyozoea na rasilimali nyinginezo. Halikadhalika wawekezaji hawa wamesababisha

²⁸ Tanzania Daima Aprili 7, 2011

²⁹ Majira Agosti 31, 2011

³⁰ Nipashe Julai 22, 2011

uhasama baina yao na wananchi kwa kushindwa kutekeleza ahadi za kushirikiana na wananchi walizotoa wakati wa kuchukua maeneo kutoka kwa wananchi³¹.

Katika hali inayoonesha kuwa kukithiri kwa migogoro ni tatizo kwa usalama wa nchi na maendeleo kwa ujumla. Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliilaumu serikali kuwa inahusika katika ongezeko la migogoro ya ardhi. Sababu kubwa iliyotajwa na Wabunge hawa ni kwa serikali kuchelewa kutoa maamuzi juu ya matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza kati ya wafugaji na wakulima kwa upande mmoja na wawekezaji kwa upande mwingine. *“Inasikitisha kuona kila mwaka serikali inaunda tume kuchunguza matatizo ya ardhi wakati hakuna majibu ya ufasaha kwa wananchi”* alihoji Mbunge Regia Mtema³². Wakati Wabunge wakitoa angalizo kwa serikali, kwenye kijiji cha Mrito wanavijiji zaidi ya 2,000 waliomba serikali kuingilia kati mgogoro baina yao na wawekezaji waliopora zaidi hekta 300 za ardhi ndani ya kijiji chao. Wanavijiji hao wanalalamika kuwa wawekezaji hao walipata ardhi hiyo katika taratibu zisizoeleweka³³. Ushirikishwaji duni wa wananchi katika masuala yanayohusu ardhi inayowazunguka umeendelea kusababisha migogoro. Kwa mfano wananchi katika eneo la Seka Suguti, wilayani Musoma Vijijini walilalamika kuwa kampuni ya Utafiti wa dhahabu kutoka Russia ya Mining Management Group (MMG) imekuwa inafanya utafiti wake pasipo kuzingatia suala zima la uhifadhi wa mazingira na afya za wakazi wa eneo hilo³⁴.

c. Migogoro ya mipaka baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi

Kwa mwaka 2011 kuliripotiwa migogoro mingi ya ardhi iliyohusisha masuala ya mipaka baina ya makundi mbalimbali. Kuna migogoro ya kimpaka baina ya vijiji na vijiji, migogoro baina ya hifadhi na vijiji pamoja na migogoro baina ya taasisi za kiserikali na wananchi mbalimbali. Migogoro hiyo iliyoibuka ni pamoja na

Mgogoro wa mpaka baina ya hifadhi ya taifa ya Mikumi na wananchi waishio kando kando ya hifadhi hiyo katika kata za Mikumi na Ruhembe umezidi kushika kasi. Mgogoro huo ambao una sababishwa kwa upande mmoja na ongezeko la ardhi kwa mahitaji ya shughuli mbalimbali za kibinadamu ikiwemo makazi³⁵. Vile vile katika wilaya ya Mbinga kuliripotiwa mgogoro wa mpaka baina ya wananchi na hifadhi ya Liparamba. Mgogoro huo ambao uliripotiwa kusababishwa na zoezi la serikali la kuipima ardhi ya hifadhi hiyo jambo ambalo wananchi wa vijiji jirani na hifadhi hiyo wanasema limevamia

³¹ The Citizen Februari 17, 2011

³² Nipashe Julai 25, 2011

³³ The Guardian Januari 15, 2011

³⁴ Nipashe Septemba 28, 2011

³⁵ Tanzania Daima Agosti 2, 2011

maeneo yao³⁶. Halikadhalika viongozi wa kata ya Ruiwa wilayani Mbarali wameingia kwenye mgogoro mkubwa kutokana na ugomvi wa mipaka baina ya vijiji vya Ruiwa, Ijumbi na Udindilwa kukithiri³⁷.

d. Ufanyaji kazi wa vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi

Sheria ya ardhi ya vijiji namba 5 ya 1999 na sheria ya utatuzi wa migogoro ya ardhi namba 2 ya 2002 zimetamka uundwaji wa mabaraza na mahakama za utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini. Utekelezaji wa majukumu wa vyombo hivi una sura nyingi, kwa upande mmoja kuna sura ya mafanikio na kwa upande wa pili kuna kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo hali inayopelekea kuongezeka kwa migogoro ya ardhi nchini. Uhalisia uliionekana kwa mwaka wa 2011 ni kwa vyombo hivi kushindwa kwa kiasi fulani kutekeleza majukumu yake ipasavyo:

Katika gazeti la Majira la Septemba 25, 2011 kulikuwa na makala ambayo ilikuwa na kichwa cha habari *“Miaka 50 ya uhuru: Mabaraza ya ardhi na nyumba bado yanakabiliwa na changamoto”*, katika makala hii mwandishi anainisha mapungufu yaliyoko katika mfumo, uundwaji na utendaji kazi wa vyombo hivi. Katika mfumo hasa katika ngazi ya kijiji mabaraza ya ardhi ya vijiji yalionekana kukosa mvuto kwa wananchi kutokana na uundwaji wake wakati mwingine kuwa na wajumbe wasiotambua masuala muhimu katika ardhi hali inayopelekea kuibuka upendeleo katika utatuzi wa migogoro.

Pia mwingiliano wa kimamlaka baina ya vyombo vya serikali na mabaraza kulipelekea mabaraza haya kushindwa kutekeleza kazi zake ipasavyo. Vile vile uundwaji wa polepole wa mabaraza ya ardhi na nyumba na wilaya katika wilaya na kanda nchini, mpaka mwaka 2011 kulikuwa na mabaraza 42 pekee nchi nzima³⁸ hali iliyopelekea mrundikano wa kesi nyingi hivyo wananchi wengi kushindwa kupata haki zao kutokana na umbali uliopo kutoka katika vijiji vyao. Changamoto nyingine iliyokumba mabaraza haya ni pamoja uelewa mdogo walionao wananchi kwenye sheria za ardhi suala ambalo linatoa wakati mgumu wakati wa utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Uelewa mdogo wa sheria unathibitishwa na habari iliyoripotiwa kwenye gazeti la (Majira Julai 15, 2011) ambayo inaainisha vyanzo vya migogoro hiyo kuwa ni kwa viongozi na wananchi kutozingatia sheria na kanuni za matumizi bora ya ardhi hasa katika maeneo ya pembezoni mwa miji na vijijini. Suala muhimu kwa wananchi na viongozi hawa ni wao kuchukua jukumu la kujifunza na kufahamu sheria za nchi juu ya suala zima la umilikishwaji wa ardhi katika maeneo yao. Kutokufahamu sheria kumepoleleka kuibuka

³⁶ Nipashe Novemba 6, 2011

³⁷ Mwananchi Machi 15, 2011

³⁸ Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2011

kwa kundi la matapeli ambao wamejiingiza katika uuzwaji wa ardhi za vijiji na maeneo ya pembezoni mwa miji mikubwa³⁹. Matapeli hawa ambao wamegundua ardhi ni mtaji mkubwa wamekuwa wanatafuta wateja zaidi ya mmoja na kuingia mikataba feki na watendaji wa vijiji jambo ambalo linachangia kuibuka migogoro mingi ya ardhi.

Kutokana na utendaji mbovu wa mabaraza haya ya ardhi, lawama nyingi zimeibuka na wakati mwingine wananchi na baadhi ya viongozi wa serikali kuchukua maamuzi ambayo sio sahihi kwa mujibu wa sheria. Kwa mfano huko Mkoani Rukwa, wakazi wa Tarafa ya Mpimbwe wilayani Mpanda walilivunja Baraza la Kata kutokana na madai kuwa wajumbe wake sio waadilifu na wasiotii sheria zilizopo katika kutoa maamuzi sahihi. Pia waliwatuhumu wajumbe hao kuwa waomba rushwa wakati wa kutoa maamuzi jambo ambalo linachochea kuibuka kwa migogoro mara kwa mara⁴⁰.

Uamuzi wa wananchi hawa ni sawa na maamuzi yaliyochukuliwa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Bwana Simbakalila ambaye aliamrisha polisi na maafisa usalama wa mkoa kumtoa ndani kwa nguvu Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya kutokana na Mwenyekiti huyo kupinga matakwa ya mara kwa mara ya Mkuu huyo wa Mkoa⁴¹. Hali hii pia imetokea huko Simanjiro Mkoani Manyara ambapo Kamati ya Maendeleo ya Kata katika kata ya Mererani ililisimamisha Baraza la Kata kutokutua migogoro ya ardhi kutokana na kile kilichodaiwa kupindisha haki pamoja na kumaliza muda wake⁴².

Ni ukweli ulio wazi kuwa si viongozi wote katika ngazi zote ambao wanaweza kufurahishwa na maamuzi yanayotolewa na mabaraza haya. Hii ni kutokana na mabaraza haya wakati mwingine kuwazuia viongozi kutimiza mahitaji yao kwa manufaa yao wenyewe na yasiyokuwa na tija kwa wananchi. Ndio maana wakati mwingine maamuzi yanayochukuliwa na Vyombo vya utawala dhidi ya mabaraza haya yanaonekana kuwa ni sehemu ya mpango wa kuyadhoofisha. Athari za kuingilia uhuru wa vyombo hivi vya maamuzi ni kupunguza morali ya ufanyaji wake wa kazi na zaidi kuondoa imani kwa wananchi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wanavitumia katika kutatua migogoro inayowakabili.

Kutokana na kuongezeka kwa migogoro ya ardhi hoja mbalimbali kutoka kwa wanasiasa, watendaji wa serikali na wananchi zilisikika kwa mwaka 2011. Mojawapo ya hoja hiyo ilikuwa ni kuvunjwa kwa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Hoja ya kuvunjwa kwa Mabaraza hayo na kuondolewa kwenye mfumo wa utatuzi wa migogoro

³⁹ Mapinga village in Bagamoyo Fact Finding Mission Report

⁴⁰ Nipashe Januari 15, 2011

⁴¹ Nipashe April 17, 2010

⁴² Mwananchi Mei 15, 2011

ya ardhi nchini ilitokana na utendaji mbovu wa baadhi ya Mabaraza haya na uundwaji husioridhisha wa Mabaraza haya katika wilaya na kanda ambazo hazina Mabaraza haya mpaka sasa. Katika kujibu hoja hizo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilitoa tamko la kupingana na mapendekezo hayo kutokana na kile ilichosema kuwa mabaraza haya ni muhimu sana katika utatuzi wa migogoro ya ardhi na yameonyesha mafanikio makubwa. Wizara ilisema kuwa suala la muhimu ni kupambana na changamoto zinazoyakumba mabaraza haya na kuongeza kasi ya uundwaji wa Mabaraza kulingana na uwezo wa bajeti ya serikali⁴³.

Suala la kuboreshwa kwa mabaraza ya utatuzi wa migogoro linaonekana kuwa ndio hoja ya msingi zaidi kuliko kuyavunja. Mfano uko wilayani Ukerewe wajumbe wa mabaraza ya vijiji, kata na wilaya walitoa maombi yao kwa serikali na asasi za kiraia kuwawezesha wao kupata mafunzo juu ya sheria za ardhi na taratibu za utatuzi wa migogoro ili kupambana na changamoto wanazokumbana nazo wakati wa utekelezaji wa majukumu yao⁴⁴. Kushindwa kutambua majukumu yao kumepelekea baadhi ya wajumbe wa mabaraza haya kuingia katika matatizo makubwa mojawapo ikiwa ni kuomba na kupokea rushwa. Mfano katika wilaya ya Kinondoni, wajumbe watatu wa Baraza la Kata la Kwembe walitiwa mbaroni na Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya Tsh. 200,000/=. Wajumbe hao walituhumiwa kuomba kiasi hicho cha fedha kutoka kwa mmoja wa watu wawili waliouziwa kiwanja kimoja kwa wakati mmoja⁴⁵.

e. Nafasi ya wanasiasa na watendaji wa serikali katika migogoro ya ardhi

Nafasi ya viongozi, wanasiasa, madiwani na wabunge pamoja na ya watendaji mbalimbali wa serikali kuanzia ngazi ya serikali za mitaa hadi serikali kuu ni kubwa sana katika migogoro ya ardhi. Nafasi hii iko katika sehemu kuu mbili, kwanza ni wao kutumia nafasi zao katika kuongeza na kuchochea migogoro ya ardhi na pili ni kupunguza na kumaliza kabisa migogoro ya ardhi. Kwa mwaka 2011 nafasi za wanasiasa na watendaji hawa zilionekana katika ngazi zote mbili kama ifuatavyo.

Viongozi wa vyama vya siasa wilayani Hanang' mkoani Manyara walilalamikiwa kuwa chanzo cha migogoro ya ardhi ambayo inaweza kupelekea kuvunjika kwa amani na utulivu kutokana na kutoa kauli za upendeleo. Lawama hizo zilitoka kwa wakulima wanaojihusisha na kilimo cha umwagiliaji katika ziwa Basotu. Wakulima hao walisema kuwa kuna kikundi cha wanawake wa Kitatoga wanaotumia nguvu ya wanasiasa ili

⁴³ Nipashe Julai 30, 2011

⁴⁴ Agosti 31, 2011

⁴⁵ Tanzania Daima Septemba 28, 2011

waondoke katika eneo hilo kwa madai ya kumpigia Mungu wao kelele ambaye wanaamini yupo katika ziwa hilo⁴⁶.

Naye mwanaharakati wa masuala ya ardhi kutoka wilaya ya Kilombero Ndugu Clavery Mwakinyonge wa kijiji cha Mkangawalo aliilaumu serikali kwa kuthamini wageni kuliko wazawa jambo linalopelekea kusababisha migogoro baina ya wawekezaji na wananchi. Akizungumza kwenye Tamasha la Jinsia lililoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) mwezi wa Septemba 2011 alisema *“Kuna mwekezaji anayetumia dawa za kuulia magugu katika shamba lake na kuathiri mashamba mengine yanayomzunguka pasipo serikali kutoa tamko lolote”*⁴⁷. Nao Wenyeviti wa serikali za mitaa katika kata ya Chanika walimkataa Mtendaji wa Kata hiyo Bwana Chalse Kapongo kwa madai ya kuwa yeye ndiye chanzo cha migogoro ndani ya eneo hilo kwa muda mrefu. Mtendaji huyo alilalamikiwa kwa tabia yake ya kujichukulia maamuzi juu ya masuala ya ardhi pasipo kuwashirikisha viongozi wa vijiji na wananchi kwa ujumla⁴⁸.

Habari za wanasiasa na viongozi wa serikali kuonekana kuwa chanzo cha migogoro ya ardhi zilizidi kuripotwa kwa mwaka 2011. Huko mkoani Morogoro wakulima na wafugaji waliwalalamikia wanasiasa kwa kuchangia migogoro kutokana na kushindwa kutekeleza ahadi wanazozitoa wakati wa kampeni za kuomba uongozi. Shutuma hizo zilitolewa na Katibu wa wafugaji mkoa wa Morogoro Ndugu Julius Megirory aliyesema *“Jamii yenyewe inaishi kwa amani, lakini wanasiasa wanapandikiza chuki ili kupata madaraka na hatimaye kusababisha machafuko”*⁴⁹.

Katika hali inayoonyesha tabia ya wanasiasa kujiingiza katika masuala ya ardhi pasipo kuwa na utafiti wa kutosha na kutoa kauli ambazo zinaweza kuwa kichocheo cha migogoro. Mgogoro wa ardhi katika eneo la Mabwepande Jijini Dar es Salaam uliingiliwa na kauli za wanasiasa zaidi ya wataalamu wa masuala ya ardhi wa Halmashauri ya Manispaa. Mgogoro huo umekuzwa kiasi cha kupelekea machafuko kutokea kutokana na viongozi wa vyama tofauti vya siasa kutoa matamko yanayopingana ambayo siyo ya kitaalamu bali ya kisiasa jambo linaloukuza migogoro huo zaidi ya kumaliza. Eneo hilo linalodaiwa kuvamiwa na wageni ambao wanatajwa hadi kuingia katika maeneo yaliyotengwa kwa makaburi, huku wazawa wakiwa hawajui hatima yao⁵⁰.

⁴⁶ Majira Januari 1, 2011

⁴⁷ Mwananchi Septemba 15, 2011

⁴⁸ Majira Julai 24, 2011

⁴⁹ Majira Agosti 1, 2011

⁵⁰ Mwananchi Septemba 12, 2011

Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nao waliilaumu Wizara ya Ardhi kuwa ndio chanzo cha kuongezeka kwa migogoro ya ardhi nchini kutokana na kuwapendelea wawekezaji zaidi. Mbunge wa Mkinga Mhe. Dustan Kitandula aliilaumu serikali kwa kutoa ardhi kubwa inayokadiriwa kuwa hekari 25,000 kwa kampuni ya Kiitaliano ya Arkadia kwenye baadhi ya vijiji vya wilaya ya Mkinga. Naye Mbunge wa Bariadi Mashariki Mhe. John Cheyo alisikitika kuwa wananchi wanaporwa ardhi yao na kupewa matajiri wachache na wale wanaojiita wawekezaji kwa mgongo wa baadhi ya watendaji wa serikali. Wabunge pia walishauri kufanyike mpango bora wa matumizi ya ardhi kwa nchi nzima kwa lengo la kutambua ukubwa wa ardhi ili pia kuweze kupatikana ardhi kwajili ya benki ya ardhi na kuondoa tabia ya wawekezaji kwenda vijijini moja kwa moja kudanganya wananchi⁵¹.

Kwa upande mwingine wanasiasa na watendaji wa serikali wanaweza kuwa sehemu muhimu sana katika kutatua migogoro ya ardhi katika nafasi zao za kiutawala kwa uadilifu. Mfano mzuri ni Mbunge wa Korogwe Vijijini Mhe. Steven Ngonyani aliyefanikiwa kutatua mgogoro wa kugombea ardhi baina ya wakazi wa kijiji cha Kwashemshi na mwekezaji wa mashamba ya mkonge ya Kwashemshi Estate. Mgogoro huo uliodumu kwa muda wa miaka minne sasa ulimalizika kwa masharti ya wananchi hao kuendelea kutumia maeneo hayo kutunza mahindi yaliyopo hadi Julai mwaka 2011 halafu shamba lirejeshwe kwa mwekezaji kwa taratibu nyingine⁵². Nao wananchi wa Kata ya Tangasisi kwa kutambua umuhimu wa watendaji wa serikali walimuomba Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Profesa Anna Tibaijuka kuwasaidia kupata haki yao baada ya kunyang'anywa maeneo yao ya makazi, ufugaji na kilimo ili kumpisha mwekezaji kujenga huduma za kijamii katika eneo hilo tangu mwanzoni mwa mwaka 2010⁵³.

f. Uelewa duni wa sheria za masuala ya ardhi

Katika hali inayoonyesha kuwa wananchi walio wengi bado wanahitaji elimu kuhusiana na sheria za ardhi nchini. Mwaka 2011 kuliibuka matukio na masuala mengi ambayo yalionekana dhahiri kuwa kuna ukosefu mkubwa wa uelewa wa sheria.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni Charles Kenyela alishangazwa na tabia ya wananchi wa Manispaa hiyo kupeleka migogoro ya ardhi polisi wakati sio sahihi kwa mujibu wa sheria. Kamanda huyo alizungumzia kuwa vituo vya polisi vimekuwa vikipokea migogoro hiyo mara kwa mara pamoja na kuwa wamekuwa wakiwashauri kupeleka migogoro hiyo katika mabaraza maalumu yaliyoundwa kusikiliza na kutoa

⁵¹ The Guardian Agosti 16, 2011

⁵² Nipashe Machi 22, 2011

⁵³ Mwananchi Septemba 12, 2011

maamuzi ya ardhi⁵⁴. Katika Manispaa ya Temeke nako kulitokea sakata la serikali ya mtaa wa Mbutu kutaka kufikishwa mahakamani kwa kosa la kugawa hekari 90 za ardhi za familia moja ambazo zilikuwa ni kati ya hekari 180 zilizoachwa kama urithi⁵⁵.

Vile vile wilayani Karatu, mkoani Arusha wananchi wapatao 308 wa kijiji cha Qangended walitishia kutumia nguvu kugawana mashamba na viwanja vilivyotolewa na serikali ya kijiji chao. Mwenyekiti wa kijiji hicho Bwana Thomas Darabe alisema kuna kila dalili za kuvunjika kwa amani katika kijiji hicho kama baadhi ya watu wataendelea kupinga maamuzi halali ya Mkutano Mkuu wa kijiji ambao uko kwa mujibu wa sheria ya serikali za mitaa ya mwaka 1982 na pia kupata uhalali wa kufanya maamuzi ya ardhi kupitia sheria ya ardhi ya vijiji ya mwaka 1999⁵⁶.

g. Madhara ya migogoro ya ardhi

Kama ilivyo ada kwenye migogoro ya aina yoyote ile ambayo hatima yake ni madhara ambayo mara nyingi yamekuwa ni hasara kwa makundi yanayohusika katika mgogoro husika. Katika mwaka 2011 madhara mbalimbali yaliripotiwa kutokana na migogoro ya ardhi kama ifuatavyo.

Wakazi wawili wa kijiji cha Lumango kata ya Kidodi Tarafa ya Mikumi wilayani Kilosa walidaiwa kuuawa na askari wa hifadhi ya Mikumi kutokana na madai ya kuingia na kufanya shughuli katika hifadhi hiyo bila kibali rasmi. Watu hao waliuawa mwezi wa Septemba mwaka 2010⁵⁷. Katika Tarafa ya Legosereti, mkoani Manyara wananchi walilalamikia kupigwa risasi kwa mwanakijiji mwenzao na askari wa kampuni inayofahamika kama Jery Farm⁵⁸. Migogoro ya ardhi imepelekea uvunjifu wa amani katika maeneo mbalimbali, mfano mapigano yaliyozuka kugombea eneo linalokadiriwa kuwa la hekari 104 lililoko eneo la Wazo, wilaya ya Kinondoni linalodaiwa kumilikiwa na mtu aliyelitelekeza toka mwanzoni mwa miaka ya 2000 na baadae kuvamiwa na wananchi wengine. Mapigano hayo baina ya mabaunsa waliotumwa na mtu anayedaiwa kulitelekeza eneo hilo na wananchi waliovamia yalipelekea vifo vya watu wawili. Matukio haya yanaendelea kuthibitisha kuwa migogoro ya ardhi ni janga la kitaifa inayohitaji jitihada za makusudi katika kuitatua kwa haraka⁵⁹.

⁵⁴ Nipashe Julai 21, 2011

⁵⁵ Tanzania Daima Julai 26, 2011

⁵⁶ Mwananchi Julai 29, 2011

⁵⁷ Nipashe Januari 15, 2011

⁵⁸ The Guardian Septemba 23, 2011

⁵⁹ Tanzania Daima Aprili 9, 2011

Halikadhalika migogoro ya ardhi imeripotiwa kurudisha maendeleo ya wananchi nyuma kutokana na kusimama kwa shughuli za kimaendeleo katika maeneo yenye migogoro hiyo. Kwa mfano mgogoro ulioripotiwa kuendelea baina ya Jumuiya ya Hifadhi ya Jamii (WMA) wilayani Serengeti kutokana na vijiji vilivyoko katika Jumuiya hiyo vya Nyichoka, Natta, Makundusi, Park Nyigoti na Ikoma Robanda kutolipwa pesa zake kwa kipindi cha mwaka mmoja. Kusitishwa kwa malipo hayo kumepelekea kusimama kwa shughuli za maendeleo ambazo zilikuwa zinategemea malipo hayo⁶⁰.

III. UVAMIZI WA ARDHI

Uvamizi wa ardhi nchini umekuwa ukishika kasi siku hadi siku katika maeneo mbalimbali nchini. Uvamizi huu ambao unasabishwa na ongezeko la thamani ya ardhi hasa katika maeneo ya pembezoni mwa majiji na miji, pia ongezeko la watu katika maeneo mbalimbali ya nchi ni sababu nyingine ikiwemo uwekezaji kwa shughuli mbalimbali. Kutokuendelezwa kwa mashamba na viwanja nako kunachangia baadhi ya watu kujinyakulia maeneo hayo. Vile vile utendaji mbovu wa baadhi ya viongozi wa serikali katika wizara na halmashauri za wilaya na manispaa husiozingatia taratibu zilizoainishwa katika sheria kwa lengo la kujipatia faida. Kwa mwaka 2011 habari mbalimbali kuhusiana na uvamizi wa maeneo nchini ziliripotiwa kama inavyoonesha hapa chini:-

Wilayani Bagamoyo katika kijiji cha Mapinga kuliripotiwa kukithiri kwa vitendo vya baadhi ya wananchi kuvamia maeneo na kujimilikisha kinyume cha sheria. Mfano shamba lililotambulika kuwa mali ya mtu mmoja aliyetambulika kwa jina la Lyatuu kuvamiwa na zaidi ya watu wapatao 1,000 waliosadikiwa wanatokea jijini Dar es Salaam. Tabia ya kuvamiwa kwa maeneo katika wilaya ya Bagamoyo imeongezeka kutokana na baadhi ya viongozi wa halmashauri za vijiji wasiokuwa waadilifu kwa kushirikiana na baadhi ya matapeli wanaoibuka kuuza mashamba kinyume cha sheria⁶¹. Ni kutokana na kukithiri uko kwa uvamizi wa mashamba ambapo gazeti la (Majira, 25/7/2011) liliripoti kuswekwa ndani kwa saa 24 kwa viongozi wa serikali ya kijiji cha Mapinga kwa amri ya Mkuu wa Wilaya kwa madai ya kuhusika katika kushawishi wananchi kuvamia shamba lenye hekari 239 lenye mmiliki halali. Ingawa kwa upande wa pili wananchi wa kijiji cha Mapinga walilalamika kuwa eneo walilovamia limekuwa kero kwao kwa muda mrefu kutokana na kuwa pori lenye wanyama ambao wanahatarisha maisha yao hasa nyakati za usiku wanapokuwa wanatokea kwenye

⁶⁰ Mwananchi Februari 2, 2011

⁶¹ Majira Julai 29, 2011

shughuli za kutafuta maisha. Habari za uvamizi ziliripotiwa pia kutokea katika kijiji cha Bwilingu katika wilaya hiyo hiyo ya Bagamoyo⁶².

Jijini Dar es Salaam uvamizi wa maeneo ulikithiri sana kwa mwaka 2011, hii ikiwa ni pamoja na maeneo ya wazi kuvamiwa kwa kasi kubwa. Katika eneo la kata ya Mabwapande nje kidogo ya jiji wavamizi waliingia na kukalia maeneo ambayo Wizara ya Ardhi mwanzoni mwa mwaka 2010 iliyachukua kutoka kwa wananchi waliokuwa wakiishi kihalali na kuwalipa fidia. Lakini katika hali ya kushangaza mwaka 2011 maeneo hayo yaliingiliwa na watu wengine ambao walianza kujenga makazi ya kudumu pasipo kuchukuliwa hatua yoyote na serikali⁶³. Habari nyingine iliyoibuka ni ile ya Manispaa ya Kinondoni kutupiwa lawama na uongozi wa mtaa wa Shekilango kwa kushindwa kumuondoa mvamizi wa eneo la wazi katika eneo hilo ambalo ameingia kinyume cha sheria⁶⁴.

Katika wilaya ya Temeke, wakazi wa mtaa wa Liganga walimwomba Waziri wa Ardhi Profesa Anna Tibaijuka kumwondoa mvamizi wa uwanja wa wazi katika eneo hilo aliyejenga kituo cha mafuta. *“Hili ni eneo la wazi na mara zote tumekuwa tunalitumia kupumzikia, manispaa ilipokuja kujenga ofisi za kata tulikubali kwa sababu ni suala la maendeleo yetu lakini ghafla tunashangaa kuona kituo cha mafuta”*, alisema mwananchi mmoja Juma Kitika⁶⁵. Nao wakazi wa mtaa wa Kilimahewa, Benaco Salasala jijini Dar es Salaam waliwalalamikia Maafisa Ardhi wa Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na uongozi wa mtaa kutaka kuuza eneo lao la makazi kwa mwekezaji wa kigeni⁶⁶.

Uvamizi wa fukwe jijini Dar es Salaam ulizidi kuongezeka kwa kasi kwa mwaka 2011 jambo linaloanishwa na ongezeko la rushwa na ufisadi. Kwa mujibu wa makala katika gazeti la (Nipashe Mei 31, 2011), uvamizi wa fukwe pembezoni mwa Bahari ya Hindi ambazo kisheria zinatakiwa kuwa huru kwa kila Mtanzania, ni uvamizi unaosababishwa na ongezeko la rushwa. Wafanyabiashara wakubwa wanaochukua maeneo haya na kujenga mahoteli makubwa pasipo uoga wowote wakati ni kinyume cha sheria ni jambo linalotia shaka kuhusu mustakabali wa rasilimali za nchi. Katika kuonyesha kuwa uvamizi ndani ya jiji la Dar es Salaam unakua kwa kasi, Mbunge wa Ilala, Mhe. Idd Azzan Zungu aliwashambulia vigogo wanaojilimbikizia ardhi kubwa ndani ya jiji.

⁶² Majira April 7, 2011

⁶³ Nipashe Julai 25, 2011

⁶⁴ Tanzania Daima Julai 27, 2011

⁶⁵ Mwananchi Septemba 1, 2011

⁶⁶ Nipashe Mei 31, 2011

Mbunge huyo alitoa rai kwa serikali kutunga sheria maalum ambayo itawabana watu wenye tamaa ya kumiliki idadi kubwa ya viwanja⁶⁷.

Katika wilaya ya Kahama kuliripotiwa tuhuma za Maofisa ardhi wa Halmashauri ya wilaya hiyo kumega eneo lililotengwa kwajili ya ujenzi wa chuo cha kilimo na kulelea watoto yatima. Katika hali ya kushangaza iliripotiwa kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya Bwana Eliza Bwana aliwakingia kifua maofisa wake kuwa hawajahusika na umegwaji wa eneo hilo⁶⁸. Wakati Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya akikanusha tuhuma hizo. Suala hilo hilo liliripotiwa katika sura nyingine, kuwa vigogo watatu akiwemo kiongozi wa elimu Kanda ya Magharibi na watumishi wa Halmashauri ya wilaya ya Kahama ndio waliouza eneo la mradi wa kioo cha yatima na kujipatia milioni 15 kutoka kwa mfanyabiashara mmoja⁶⁹.

Katika Manispaa ya Mtwara eneo la Mikindani iliripotiwa kuwa uzembe uliofanywa na wakuu wa idara ya ardhi na mipango miji ulisababisha uvamizi mkubwa na ujenzi holela katika Manisapaa hiyo⁷⁰. Nako mkoani Lindi katika wilaya ya Liwale, baadhi ya viongozi wa kijiji cha Kibutuka walilalamikiwa pamoja na Mbunge aliyemaliza muda wake Hassan Kigwalilo kuwa waliuza eneo la shule kwa mwekezaji pasipo kushirikisha wananchi kitendo ambacho ni kukiukwa kwa sheria ya ardhi ya vijiji namba 5, 1999⁷¹.

Gazeti la Nipashe la tarehe 26 Februari 2011, liliripoti kuwa wafugaji kutoka wilaya ya Musoma vijijini na Serengeti walivamia bonde la mto Mara na kuingiza mifugo wanaokadiriwa kufikia 30,000 baada ya maeneo yao ya malisho kuvamiwa na magugu. Bonde hilo lililopo kijiji cha Hekwe huenda likaharibiwa na makundi hayo ya mifugo na kuzidi kusababisha uharibifu wa mazingira. Kitendo cha wafugaji hao kuhamahama kunasababishwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya tabia ya nchi katika maeneo mbalimbali nchini. Katika wilaya ya Bunda, kijiji cha Sarawe wananchi zaidi ya 400 walivamia eneo la shamba lilinalogombaniwa kati yao na shule ya sekondari ya Ikizu wakiwa na silaha mbalimbali za jadi. Katika migogoro huu kila upande, wa shule na ule wa wananchi, unadai eneo ni lake. Hali hii ililileta hali ya tafrani kwa watumiaji wa eneo hilo ambao ni wananchi na watumiaji wa shule⁷².

⁶⁷ Nipashe Agosti 8, 2011

⁶⁸ Mwananchi Agosti 20, 2011

⁶⁹ Mwananchi Septemba 19, 2011

⁷⁰ Nipashe Agosti 1, 2011

⁷¹ Mwananchi Aprili 5, 2011

⁷² Majira Septemba 17, 2011

Kutokana na kukithiri kwa uvamizi katika maeneo mbalimbali nchini, serikali kupitia Wizara ya Ardhi kwa mwaka 2011 imekuwa ikinukuliwa na vyombo ikikemea vitendo hivi vya kivamizi. Mwezi Septemba 2011, Waziri wa Ardhi Profesa Anna Tibaijuka aliwataka watumishi katika sekta ya ardhi wanaoyumbisha sheria na kanuni kwa makusudi wajiondoe wenyewe kabla ya kufukuzwa. Profesa Tibaijuka alisema “*Kwa masikitiko makubwa napenda kutamka kuwa kwenye ofisi zetu kuna udhaifu mkubwa katika utekelezaji wa sheria hizi; Ni dhahiri kuwa Watanzania wanataka huduma bora hawataki migogoro ya ardhi, wanachukia huduma zilizo chini ya kiwango, wanataka kufaidika na ardhi yao pale inapotwaliwa kwa matumizi ya serikali au uwekezaji wa aina yoyote*”⁷³. Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rehema Nchimbi aliwataka watumishi wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) kuwa waaminifu katika utendaji wao na kuacha tabia ya kujilimbikizia viwanja⁷⁴.

Wakati huo huo iliripotiwa kuwa Wizara ya Ardhi ilitoa nafasi kwa wale wote waliovamia maeneo ya wazi kuondoka wenyewe ili kuruhusu maeneo hayo kutumika kwa manufaa ya wananchi wote kama ilivyo makusudio ya maeneo hayo. Wizara ilitamka wazi kuwa kwa wale watakaoshindwa kuondoka kwa hiari yao, serikali itachukua jukumu la kubomoa majengo yote yaliyojengwa katika maeneo hayo⁷⁵.

IV. BOMOABOMOA, UHAMISHWAJI KATIKA ARDHI NA FIDIA YA ARDHI KWA WANANCHI

Nchini Tanzania ardhi ni mali ya umma chini ya usimamizi wa serikali, kwa maana hiyo serikali ina mamlaka ya kuchukua eneo lolote nchini na kulitumia kwa kile kinachoitwa kwa manufaa ya umma. Ni mara kwa mara kumekuwa kukiripotiwa taarifa za maendelezo yanayofanywa kwenye ardhi na serikali ambayo yamekuwa yanahusishwa na wananchi kuvunjiwa nyumba zao, kuondolewa kwenye ardhi wanazozitumia kwa makazi na kilimo. Kwa mujibu wa sheria ya ardhi namba 4 ya mwaka 1999, wananchi wanastahili fidia pale ambapo eneo wanaloishi wanaishi kihalali. Vile vile kutokana na uwekezaji kutajwa kuwa sehemu ya “manufaa ya umma” basi pale wananchi wanapoondolewa kupisha uwekezaji watatakiwa kulipwa fidia.

Kwa mwaka 2011 habari mbalimbali kuhusiana na bomoabomoa za nyumba za wananchi kupisha upanuzi wa barabara, wananchi kuhamishwa kupisha uwekezaji

⁷³ Majira Septemba 27, 2011

⁷⁴ Nipashe Septemba 26, 2011

⁷⁵ Nipashe Septemba 26, 2011

pamoja na ulipwaji wa fidia ziliripotiwa kwa kiasi kikubwa kama inavyochambuliwa hapa chini.

Katika jiji la Dar es Salaam iliripotiwa kuwa wakazi wa Chang'ombe waliulalamikia uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Temeke kwa kuweka alama za kubomoa nyumba zao bila ya kulipwa fidia ili kupisha ujenzi wa barabara⁷⁶. Nao wakazi wa Kigilagila ambao kwa muda mefu nyumba zao zilikuwa kwenye mpango wa kubomolewa ili kupisha upanuzi wa uwanja wa kimataifa wa ndege wa Julius Nyerere (JNIA) walianza kulipwa fidia zao lakini kukiwa na manung'uniko kuwa fedha wanayolipwa ni kidogo sana. Wananchi hao wanalalamika kuwa fedha wanayolipwa haiendani na gharama za ujenzi wa sasa kutokana na ukweli kuwa tathimini ya nyumba na mali nyingine ilifanyika mwaka 1997. Halikadhalika wananchi hao walilalamikia udogo wa viwanja mbadala wanavyopewa jambo litakalosumbua wakati wa ujenzi⁷⁷.

Nao wakazi wa maeneo ya Mbezi Juu barabara ya Goba eneo la Samaki Wabichi waliitaka serikali kuwa wazi na kuwashirikisha wananchi katika kila hatua katika kufanya maendeleo kwenye maeneo yanayokaliwa na wananchi. Wananchi hao walitoa angalizo hilo walipokutana wakati wa kujadili tishio la kukumbwa na bomoabomoa ya upanuzi wa barabara ya Bagamoyo itakayounganishwa na barabara ya Morogoro eneo la Mbezi mwisho⁷⁸. Pia iliripotiwa kuwa wakazi wa Kipawa na Ukonga Jijini Dar es Salaam walitarajiwa kukumbwa na bomoa bomoa ili kupisha upanuzi wa barabara ya mabasi yaendayo kwa kasi⁷⁹. Vile vile katika hali inayoonyesha kukosekana kwa Ushirikishwaji hafifu wa wananchi katika mipango ya maendeleo inayotekelezwa na serikali. Mahakama Kuu ya Tanzania ilitoa fursa kwa wakazi wa Kata ya Kinyerezi na Manispaa ya Ilala kutafuta ufumbuzi wa migogoro ulioibuka baada ya Manispaa hiyo kutoa tangazo la kupima viwanja katika eneo hilo bila ya makubaliano na wakazi hao⁸⁰.

Katika mikoa mingine kuliripotiwa habari mbalimbali kuhusiana na masuala ya fidia kama vile mkoani Pwani ambako wakazi wa eneo la Mkata walitishia kuzuia ujenzi wa barabara ya Mkata – Handeni kutokana na kukosekana makubaliano ya ulipwaji fidia. Wananchi hao ambao mwaka 2010 wakati mradi unaanza waliahidiwa kulipwa fidia walisikitishwa na kauli ya TANROADS makao makuu kuwa hakuna mpango wa

⁷⁶ Majira Julai 27, 2011

⁷⁷ Nipashe Januari 1, 2011

⁷⁸ Mwananchi Machi 22, 2011

⁷⁹ Mwananchi Septemba 20, 2011

⁸⁰ Nipashe Septemba 28, 2011

kuwalipa fidia wananchi hao kutokana na kuwa walivunja sheria kwa kujenga katika eneo la hifadhi ya barabara⁸¹.

Mkoani Arusha iliripotiwa kuwa Halmashauri ya wilaya ya Arumeru ilishindwa kutekeleza mkataba wa kulipa fidia ya Tsh. 837,550,000/= kwa kampuni ya Burka Development ili iweze kukabidhi viwanja 6,000 kwa wananchi walioomba maeneo hayo kwajili ya ujenzi wa makazi na shughuli mbalimbali za maendeleo⁸². Halikadhalika mkoani Tanga katika eneo la Amboni Mafuriko, wananchi waliotakiwa kuyahama makazi yao kupisha ujenzi wa barabara ya Tanga-Horohoro yenye urefu wa kilomita 65 wameiomba serikali kuharakisha malipo ya fidia zao kama walivyoahidiwa na Rais Jakaya Kikwete mnamo mwezi Mei 2010⁸³. Vile vile wakazi wa wilaya ya Bariadi walilalamikia serikali juu ya hatua yake ya kuvunja nyumba zao ili kupisha ujenzi wa barabara ya lami kutoka Lamadi hadi mjini Bariadi pasipo kuwalipa fidia. Wakati wananchi hao wakilalamika, Wizara ya Ujenzi ilisisitiza kutowalipa fidia kwa maelezo kuwa walijenga ndani ya hifadhi ya barabara⁸⁴.

Habari nyingine kuhusiana na fidia zilizoripotiwa kwa mwaka 2011 zilikuwa ni pamoja na serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi na Usafirishaji kutoa ahadi ya kuwalipa fidia wanavijiji wa vijiji vya Ibadakuli na Kolandoto mkoani Shinyanga ili kupisha upanuzi wa uwanja wa ndege wa Ibadakuli. Serikali ilisema kuwa itatenga jumla ya Tsh. Milioni 328 kwenye bajeti ya mwaka 2012/13 ili kulipa fidia kwa kaya 241. Lakini wananchi wa maeneo hayo waliitahadharisha kuwa tathimini ya ardhi na mali nyinginezo ilifanyika toka mwaka 2006 hali itakayosababisha fidia hizo kutokukidhi mahitaji ya sasa⁸⁵. Pia Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa kiliripotiwa kutenga jumla ya Tsh. Bilioni 8.7 kuwalipa fidia wafugaji ambao mifugo yao ilikufa kutokana na ukame uliotokea mwaka 2008/09⁸⁶.

Wakati matukio yote haya yakiripotiwa kutokea serikali ilikiri kuwa masuala ya ulipwaji wa fidia na kuhamisha wananchi kutoka eneo moja kwenda jingine yamekuwa changamoto kubwa kwa wananchi walio wengi. Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini ilikiri kuwa kuna baadhi ya watendaji wa serikali ambao wamekuwa si waaminifu kiasi cha kutumia uelewa mdogo wa wananchi juu ya sheria kuwadhulumu haki zao⁸⁷.

⁸¹ Mwananchi Julai 30, 2011

⁸² Nipashe Januari 11, 2011

⁸³ Nipashe Agosti 2, 2011

⁸⁴ Nipashe Agosti 18, 2011

⁸⁵ The Guardian Julai 29, 2011

⁸⁶ Daily News Julai 7, 2011

⁸⁷ The Guardian Julai 25, 2011

Suala hilo la watendaji wasio waadilifu linathibitishwa uamuzi wa Waziri wa Ardhi Nyumba na Makazi Profesa Anna Tibaijuka aliyeagiza zoezi la tathmini ya nyumba zitakazobomolewa katika eneo la Kurasini wilayani Temeke kupisha upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam lirudiwe upya ili kumaliza malalamiko ya wakazi hao. Waziri Tibaijuka alisema “*Utaratibu wa fidia ni lazima utazamwe upya kwakuwa inaonekana kuna watu waliopewa dhamana na Wizara lakini badala ya kufanya walichotakiwa kufanya kwa mujibu wa sheria wanaharibu*”⁸⁸.

Kimsingi kinachoonekana katika habari zote zilizoripotiwa kwa mwaka 2011 kuhusiana na masuala ya fidia, kikubwa ni ukosefu wa ushiriki wa wananchi watakaoathirika na miradi mbalimbali inayobuniwa na serikali. Vile vile suala la serikali kufanya tathmini na muda mrefu kupita kabla ya kufanya malipo ya fidia ni suala ambalo limeonekana kuwasumbua zaidi wananchi wanaohamishwa. Hii ni kutokana na kuwa thamani ya ardhi na gharama za maisha zinapanda kila mara jambo linalosababisha fidia hizo zinapokuja kulipwa kushindwa kukidhi mahitaji ya wananchi kwa wakati huo. Vile vile suala la baadhi ya watendaji wa serikali kupindisha sheria kwa manufaa yao wakati wa kufanya tathmini na wakati wa ulipwaji fidia ni suala ambalo linahitaji kukemewa kwa nguvu zote kwakuwa linajenga chuki baina ya wananchi na serikali lakini vilevile kurudisha maisha ya wananchi nyuma.

V. UWEKEZAJI KWENYE SEKTA YA MADINI

Masuala mbalimbali katika uwekezaji kwenye sekta ya madini yaliibuka kwa kiasi kikubwa kwa mwaka 2011. Masuala haya yalijikita zaidi katika migogoro baina ya makampuni ya migodi na wananchi wanaoishi jirani na migodi hiyo. Pia suala la uchimbaji wa madini ya uranium nalo liliibua mjadala mzito miongoni mwa wananchi na wadau mbalimbali.

Gazeti la Nipashe 25/7/2011 liliripoti uvamizi uliofanywa na wachimbaji wadogowadogo kandokando ya mabwawa yanayozunguka vijiji vya Songwa, Ikonongo, Maganzo na Masagala vilivyopo Mwadui. Serikali ya Wilaya ya Kishapu iliingilia kati uvamizi huo na kuwafukuza wachimbaji huo kutokana na kile kinachoaminika uharibifu wa vyanzo vya maji ambavyo ni muhimu kwa maisha ya wakazi wote. Pia suala la uchimbaji wa madini ya uranium, serikali ilipewa tahadhari kuhakikisha kuwa uchimbaji huo hausababishi madhara kwa wananchi⁸⁹. Halikadhalika Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC) lilikanusha madai ya kuwa wanavijiji wanaoishi jirani na mgodi wa North Mara waliathirika na sumu kutoka katika mgodi huo. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na NEMC ulionyesha kuwa wananchi hao waliathirika na madini kama vile mekiyuri kutoka

⁸⁸ Aprili 1, 2011

⁸⁹ Mwananchi Julai 21, 2011

katika vyanzo mbalimbali vya mito. Ripoti hiyo ya NEMC inapingana na taarifa zilizoripotiwa mwaka 2009 kuwa takribani wananchi 21 na mifugo 200 walikufa kutokana kunywa maji yaliyochanganyikana na sumu kutoka kemikali za mgodini⁹⁰.

Julai 20 2011, gazeti Mwananchi liliripoti jinsi viongozi wa dini walivyopokelewa na vilio vya wakazi wa vijiji vinavyozunguka mgodi wa Nyamongo unaomilikiwa na kampuni ya African Barrick North Mara kutokana na dhuluma waliyofanyiwa katika malipo ya fidia. Pia wananchi hao walizungumzia mahusiano mabaya yaliyopo baina ya kampuni na wao kiasi cha kuhatarisha maisha yao kila siku kutokana na ulinzi uliokithiri unaofanywa na walinzi wa mgodi huo. Hata utekelezaji wa ahadi limekuwa jambo gumu sana kwani hata hospitali ya kisasa iliyoahidiwa haijajengwa na wala hakuna umeme uliowekwa kama ahadi zilivyokuwa.

Iliripotiwa pia kuwa hatua ya Tanzania kujiunga na Mpango wa Uhamasishaji wa Uwazi katika Tansia ya Uziduaji (Extractive Industries Transparency Initiative) itasaidia kuweka uwazi na uwajibikaji katika mapato yatokanayo na maliasili za madini nchini. Hali hii itasaidia katika kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusu mchango husioridhisha wa sekta ya madini kwenye uchumi na maisha ya wananchi⁹¹.

Habari zilizoibuka ni pamoja mgogoro wa wananchi na kampuni ya madini ya mgodi wa Resolute Tanzania Limited huko Nzega kutokana na kushindwa kutoa huduma za msingi kwa wakazi wa maeneo hayo kama vile barabara, maji, ajira kwa vijana na kuongeza malipo ya mrabaha kwa Halmashauri ya wilaya⁹². Pia wachimbaji wadogowadogo katika machimbo ya Mererani waliomba serikali kuwapatia mikopo ili waweze kufanya shughuli zao za uchimbaji kwa ufasaha⁹³. Huko Tarime kuliripotiwa wananchi wanaozunguka mgodi wa North Mara kukatishwa tama kutokana na kutokutekelezwa kwa ahadi zilizotolewa na wamiliki wa mgodi huu kwa muda mrefu sasa. Ahadi hizo ni pamoja na ujenzi wa madarasa, zahanati, visima vya maji, na kulipia karo za wanafunzi⁹⁴.

Suala la uharibifu wa mazingira kutokana na uchimbaji husiozingatia utaratibu maalum ni mojawapo y masuala yaliyoiripotiwa. Katika wilaya ya Muheza kwenye kata ya Amani na Zirai⁹⁵ habari kama hii pia iliripotiwa kutoka huko Geita kwenye kijiji cha Nyaruyeye

⁹⁰ Daily News Julai 21, 2011

⁹¹ Majira Januari 14, 2011

⁹² Mwananchi Februari 9, 2011

⁹³ Nipashe Januari 4, 2011

⁹⁴ Mwananchi Machi 28, 2011

⁹⁵ Mwananchi Septemba 25, 2011

ambako wachimbaji 300 walitimuliwa kwa kuvamia eneo na kuchimba migodi kinyume cha sheria⁹⁶. Huko wilayani Arumeru iliripotiwa kuwa zaidi ya mashamba 170 yamegeuzwa kuwa machimbo ya madini hali inayopelekea uharibifu mkubwa wa mazingira. Pia hali hiyo inatishia usalama na uhakika wa chakula kwa wakazi wa maeneo haya ambao tegemeo lao kubwa ni kilimo. Maeneo yaliyoathirika zaidi ni pamoja na kata za Nkoanrua, Nkwaranga, Amureli, Mwivaro and Sasi. Uchimbaji huu pia umepelekea kupanuka haraka kwa mto Nduruma na hivyo kuharibika kwa daraja la Sasi linalounganisha vijiji vya Sasi na Amureli⁹⁷.

Suala la kuimarisha ushirikiano baina ya makampuni yaliyowekeza katika migodi na wananchi ni sehemu ya mambo yaliyoripitiwa, ambapo kampuni ya African Barrick Gold ilizindua mfuko wa maendeleo ambao utawashirikisha wananchi katika kukuza maisha yao katika maeneo ya afya, utunzaji wa mazingira, elimu pamoja na kutoa elimu ya kwa vijana katika ujasiriamali⁹⁸. Pamoja na mfuko huu kuzinduliwa na kampuni hii bado tatizo linaloonekana ni nani atafaidika na miradi itakayoibuliwa na mfuko huo. Ushiriki wa wananchi katika mfuko huu ni finyu sana kiasi ambacho wao watakuwa watu wa mwisho kwenye maamuzi. Hali hii itawapeleka kule kule kwa wao kuwa wapokeaji wa miradi ambayo si kipaumbele kwao ila kwa baadhi ya watu na kwa manufaa yao wakiwa wachache.

Suala la fidia kwa wananchi wanaotakiwa kupisha uchimbaji mkubwa wa madini ni mambo yaliyofukuta kwa mwaka 2011, ambao wananchi wa kitongoji cha Tembo katika kijiji cha Mnekezi waliahidi kuwa hawataondoka katika eneo linalomilikiwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) mpaka watakapolipwa fidia zao halali⁹⁹. Suala la siasa kutajwa kuwa kichocheo muhimu cha migogoro baina ya wananchi na wamiliki wa migodi mikubwa ni moja ya habari kwa mwaka 2011. Baadhi ya wananchi walitoa maoni kuwa wanasisia wanaingiza maneno katika migogoro hii kwa manufaa yao ya kisiasa ikiwa ni pamoja na kutaka kushinda nafasi mbalimbali za kisiasa kama vile ubunge na udiwani¹⁰⁰.

⁹⁶ Majira Septemba 23, 2011

⁹⁷ The Guardian Septemba 5, 2011

⁹⁸ The Citizen Septemba 8, 2011

⁹⁹ Nipashe Aprili 4, 2011

¹⁰⁰ Majira Agosti 14, 2011

VI. MATUMIZI YA ARDHI KWA KILIMO

Tanzania inategemea kilimo kwa kiasi kikubwa katika kukuza uchumi wake kama nchi na kwa mwananchi mmoja mmoja. Kwa maana hiyo matumizi ya ardhi kwa kilimo ni jambo ambalo halikwepeki hata kidogo. Serikali ya Tanzania imekuwa ikiibua mikakati na sera mbalimbali katika kuhakikisha kuwa wananchi wanafaidika na kilimo halikadhalika uwekezaji katika kilimo unavutia wawekezaji wengi zaidi. Kauli mbiu ya Kilimo Kwanza ni mojawapo ya hatua za karibuni kwa upande wa serikali katika kuendeleza kilimo. Pamoja na hayo kuna miradi mingine kama vile ya SAGCOT, AGRA na mingineyo ambayo yote imelenga katika kilimo. Baadhi ya mambo yaliyoibuka kwa mwaka 2011 katika sekta ya kilimo ni pamoja na:-

Wakulima katika nchi za Shirikisho la Afrika Mashariki walitakiwa kuhakikisha kuwa wanaungana na kufanya kazi kwa pamoja ili kukuza uzalishaji wao kwa kushirikishana teknolojia na mbinu mbalimbali katika kilimo. Kwa mfano vyama vya kilimo vya TASO cha Tanzania na ASK cha Kenya walitakiwa kushirikishana utaalumu¹⁰¹. Wakati huo huo MVIWATA ilitaka serikali kufungua mipaka kwa wakulima kuuza mazao yao nje ya nchi ili waweze kujipatia mapato ya uhakika kwani kwa kufunga mipaka hiyo kunawafanya wakulima wapunguze uzalishaji wa mazao kutokana na kukandamizwa na wanunuaji wa mazao wa ndani ya nchi¹⁰².

Suala la bajeti ya Wizara ya Kilimo kukwama kupita bungeni wakati wa kuwasilisha makadirio ya Wizara hiyo kwa mwaka 2011/2012 nalo lilionekana kuvuta hisia sana. Bajeti hiyo ambayo ilikuwa ni Tsh. bilioni 926 sawa na asilimia 6.7 ya bajeti ya serikali¹⁰³. Wabunge walilalamikia ufinyu wa bajeti hiyo kiasi cha kuonekana kuwa serikali bado haijawa makini katika kuhakikisha kuwa kilimo kinamkomboa mkulima mdogomdogo¹⁰⁴. Serikali ililalamikiwa kuwa bajeti hiyo haiendani na kauli mbiu ya serikali ya Kilimo Kwanza pamoja na kutokutoa kipaumbele kwa zao la pamba hali inayoonekana kuwa zao hilo linataka kutelekezwa kama zao la kahawa lilivyotelekezwa miaka ya nyuma.

Halikadhalika urasimu katika zoezi la usambazaji wa pembejeo za kilimo kupitia wakala wa usambazaji ulilalamikiwa na wakulima kuwa kumekuwepo na ucheleweshaji wa makusudi na kumfikia mkulima wakati msimu wa kilimo ukiwa umeshaanza. Kutokana na ukiritimba huo iligundulika kwa kiasi kikubwa uzalishaji umekuwa unapungua badala

¹⁰¹ Tanzania Daima, Julai 30, 2011

¹⁰² Majira Julai 25, 2011

¹⁰³ Tanzania Daima Julai 26, 2011

¹⁰⁴ Tanzania Daima Julai 26, 2011

ya kuongezeka na hali hiyo kutishia utekelezaji wa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza¹⁰⁵. Serikali inatakiwa kuchukua hatua za haraka kudhibiti hali hii ambayo kwa muda mrefu sasa imekuwa inalalamikiwa na wakulima walio wengi vijijini.

Utekelezaji wa kauli mbiu ya Kilimo Kwanza pia iliripotiwa kwa kiasi kikubwa kwa mwaka 2011. Mambo yaliyoibuka kuhusu Kilimo Kwanza ni pamoja na kulalamikiwa kwa ubora wa pawa tila zinazotolewa kwa mikopo kwajili ya kilimo. Ubora wa Vyombo hivi umelalamikiwa kuwa ni wa chini sana kiasi ambacho haustahimili udongo wa maeneo yote ya nchi. Ubora huu mdogo umeingiza wakulima wengi hasara kutokana na kuharibika mapema hata kabla ya kumalizika kwa msimu wa kilimo hali inayohatarisha ulipwaji wa mikopo¹⁰⁶. Kauli mbiu ya Kilimo Kwanza ilizidi kukosolewa kuwa haina tofauti na kauli zilizopita za serikali ambazo ziliishia katika kushindwa. Hii inatokana na ushikishwaji duni uliofanywa na serikali wakati wa kuibua kauli mbiu hii na hali hiyo inaendelea katika utekelezaji wake ambapo mkulima mdogomdogo amezidi kuwekwa pembeni. Suala la mikopo kwa wakulima wadogowadogo limeonekana kuwa ni ndoto kutokana na ukweli kuwa masharti yaliyoainishwa ni magumu sana. Pia uwezo wa wakulima hawa kununua matrekta moja kwa moja bado ni mdogo sana tofauti na kauli ya serikali kuwa wakulima wadogowadogo wangufaika¹⁰⁷.

Masuala mengine yaliyoibuka kwenye kilimo kwa mwaka 2011 ni pamoja na wilaya ya Kilombero kutenga eneo la kuzalisha bidhaa za kilimo, yaani Kilombero District Agriculture Processing Zone Project (KDAPZP). Mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa kuufanya mkoa wa Morogoro kuwa ghala la chakula la Taifa (FAMOGATA). Mradi huo utatekelezwa katika kijiji Lungongole kata ya Kibaoni ambapo eneo la hekari 200 tayari limeshapatikana. Mradi huu utasaidia kupunguza umaskini kwa wakulima na wafugaji¹⁰⁸. Vile vile kilimo cha mkataba baina ya mkulima na mnunuzi kilitajwa kuwa ndio mkombozi wa mkulima wa Tanzania kutokana kutoa uhakika wa soko kwa mazao yatakayozalishwa¹⁰⁹.

Habari za SAGCOT (Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania) na AGRA (Alliance for a Green Revolution in Africa) nazo ziliripotiwa kwa kiasi kikubwa. Wakati SAGCOT ikizungumziwa na viongozi wa serikali kuwa utakuwa kichocheo cha kilimo katika maeneo ya Kusini mwa nchi pamoja na kuongeza mtaji katika kilimo kutoka wawekezaji mbalimbali ndani na nje ya nchi. Vile vile SAGCOT itasaidia katika kukuza

¹⁰⁵ Nipashe Julai 31, 2011

¹⁰⁶ The Guardian Julai 28, 2011

¹⁰⁷ Mwananchi Agosti 28, 2011

¹⁰⁸ Nipashe Julai 30, 2011

¹⁰⁹ The Citizens Januari 16, 2011

ushirikiano na nchi majirani kama vile Zambia, Malawi na DRC Kongo¹¹⁰. Kuhusu AGRA kiasi cha Tsh. 11.4 bilioni zilitolewa kwa mwaka 2011 kwajili ya kuendeleza kilimo chini¹¹¹. Habari zote hizi za SAGCOT na AGRA zinaonekana kama mkombozi kwa wakulima wadogo wadogo lakini utekelezaji wake bado haujawa wazi kiasi cha kuhakikisha kuwa wananchi wanashiriki kwa kiasi kikubwa katika kufaidika na pesa zinazowekwa na serikali na wafadhili mbalimbali katika kukuza kilimo nchini. Ni jukumu la serikali kuhakikisha kuwa kunakuwepo na ushiriki wa wananchi wa moja kwa moja katika mikakati na mipango ya kilimo kutokana na ukweli kuwa zaidi ya asilimia 70 ya watazania wote wanategemea kilimo kwenye kukuza uchumi wao.

VII. UFUGAJI NA WAFUGAJI

Tanzania ni moja ya nchi katika bara la Afrika ambayo ina mifugo mingi, sekta ya mifugo ni mojawapo ya sekta zinazolingia serikali fedha za kigeni. Sekta hii pia imekuwa na msaada mkubwa kwa maisha ya kila siku ya Mtanzania mmoja mmoja. Pamoja na umuhimu wa sekta hii bado serikali na wadau mbalimbali wanaohusika na sekta hii hawajaipa uzito wa kutosha sekta hii na kuchukuliwa kuwa ni sekta ndogo baada ya sekta nyingine kama kilimo, madini na wanyama pori. Kwa mwaka 2011 masuala mbalimbali yaliripotiwa kama ifuatavyo:-

Kutokana na kuongezeka migogoro ya ardhi na kukosekana kwa ufugaji husio na tija nchini. Mkoa wa Arusha uliingia katika mkakati wa kuwezesha kila wilaya kuwa na ramani itakayoainisha kanda za mazao, na nyanda za malisho kwa wakulima na wafugaji. Sekta ya kilimo na ufugaji imeajiri asilimia 80 ya wakazi wa mkoa wa Arusha¹¹². Huko wilayani Ngorongoro mpango wa kujenga ranchi kubwa na ya kisasa kwa wafugaji wa maeneo hayo uliripotiwa kuwa katika hatua za awali chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Ngorongoro (NCAA). Ranchi hiyo inatarajiwa kugharimu bilioni 5/- mpaka kukamilika kwake¹¹³.

Wakati hayo yakitokea huko Arusha na Ngorongoro, huko Rufiji katika kata ya Chumbi iliripotiwa kuwa wafugaji walioko katika eneo hilo kwa sasa wanatosha na hawahitajiki wengine. Hiali hiyo inatokana na eneo lililotengwa kwajili ya mifugo kuwa limejaa¹¹⁴. Wilayani Meatu hali ilikuwa tete zaidi kutokana na wafugaji wanaoishi katika vijiji vya Lukale na Mwabagumu kuahidi kuwa wangepambana na yeyote ambaye angethubutu

¹¹⁰ Daily News Januari 14, 2011

¹¹¹ Daily News Aprili 5, 2011

¹¹² Mwananchi Julai 21, 2011

¹¹³ Daily News Aprili 5, 2011

¹¹⁴ Mwananchi Agosti 16, 2011

kuwahamisha kutoka katika eneo hilo kwa kile wanachodaiwa kuishi na kufanya shughuli zao katika eneo la hifadhi ya wanyamapori¹¹⁵.

Wakati huo huo wafugaji katika wilaya ya Kiteto walilalamikiwa kuwa wamekuwa chanzo cha wilaya hiyo kutokukua kiuchumi kutokana na tabia yao ya kuhamahama kutoka eneo moja hadi jingine kutafuta malisho¹¹⁶. Hali hiyo ya kuhama hama kwa kiai kikubwa imepelekea uharibifu wa mazingira pamoja na kushindikana kufanyika kwa kazi nyingine za kiuchumi kama kilimo na biashara. Pia wafugaji walioondolewa katika ardhi oevu kwenye bonde la Ihefu, wilaya ya Mbarali wameanza kurejea kimya kimya pasipo idhini ya serikali¹¹⁷. Wafugaji hao ambao waliondolewa miaka ya 2006/07 na kuhamishiwa mikoa ya Lindi, Pwani na Mtwara na Morogoro kwa lengo la kuhifadhi mazingira wameanza kurudi na idadi kubwa ya mifugo jambo linalotishia usalama wa bonde hilo kimazingira.

Suala la mabadiliko ya tabia ya nchi na madhara yake kwa wafugaji ni jambo ambalo kwa mwaka 2011 lilionekana kama hatari mojawapo kubwa kwa maendeleo ya ufugaji na wafugaji. Wafugaji katika maeneo mengi ya nchi wamekuwa wanalalamikia upungufu wa malisho na maji katika maeneo yao tofauti na miaka mingine. Wafugaji wengi walisema kuwa mwaka wa 2011 umeonyesha hali ya hatrai katika miaka inayokuja kutokana na hali ya kiangazi kuongezeka muda kuliko wakati mwingine wowote¹¹⁸.

Habari nyingine za wafugaji ni pamoja na wafugaji walioko ndani ya eneo la Mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro kulalamikia gawio dogo wanalopata kutoka katika Mamlaka ya NCAA la Tsh. Bilioni 1.5/- kwa mwaka. Wafugaji hao wanalalamika kuwa pesa wanayopata ni ndogo sana katika kuboresha huduma za jamii na kupambana na ukame wanaolikumba eneo hilo kwa muda mrefu¹¹⁹.

VIII. MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIA YA NCHI

Suala la mazingira ni suala nyeti sana kwa nchi kama Tanzania kutokana na utegemezi mkubwa ulioko katika mvua za majira kwajili ya kilimo na kazi nyingine. Habari za mazingira kwa mwaka 2011 ziliambatana sana na suala la mabadiliko ya tabia ya nchi. Habari nyingi ziligusia uharibifu wa mazingira kuliko zile ambazo zilionyesha jitihada za kuhifadhi mazingira. Baadhi ya habari zilizoripotiwa ni pamoja na zifuatazo:-

¹¹⁵ Nipashe Mei 17, 2011

¹¹⁶ Tanzania Daima Aprili 5, 2011

¹¹⁷ Mwananchi Januari 10, 2011

¹¹⁸ The Guardian Septemba 2, 2011

¹¹⁹ The Citizens Septemba 27, 2011

Mabadiliko ya tabia ya nchi yaliripotiwa kuwa yanakwamisha uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Baadhi ya maeneo nchini yameanza kukumbwa na uhaba wa mvua na maji hivyo kuendeleza kuharibu mfumo wa maisha wa wananchi hawa. Hali hii inahitaji hatua za haraka zaidi hasa ikizingatiwa kuwa wanavijiji wengi wanakabiliwa na ukosefu wa elimu ya utunzaji mazingira. Mabadiliko haya pia yalionekana kuanza kukumba maeneo ya mijini hasa kutokana na kuongezeka kwa hali ya joto katika miji kama Dar es Salaam, Morogoro, Arusha na kwingineko¹²⁰.

Iliripotiwa pia kuwa athari za mabadiliko ya tabia ya nchi yameanza kuonekana kwa kupungua kwa pato la taifa. Mabadiliko katika misimu ya mvua, majira tofauti ya mazao kustawi pamoja na kuathirika kwa bahari, mito na maziwa. Chanzo kikubwa kinachotajwa kuwa kisababishi cha mabadiliko haya ni pamoja na uharibifu wa mazingira, ukataji miti ovyo, utiririshaji maji machafu kutoka viwandani pamoja masuala mengine mengi¹²¹.

Wakati mabadiliko ya tabia ya nchi yakionekana kuwa ni maafa ya nchi na dunia kwa ujumla. Uko wilayani Hai katika kijiji cha Foo kata ya Machame iliripotiwa kuwa vitendo vya wananchi vya kukata na kuvuna misitu pasipo kupanda miti mingine vinaongezeka kila siku. Hali hiyo ya ukataji wa miti katika misitu hiyo kunatishia kukauka kwa vyanzo vya maji ambavyo ni vingi katika eneo hilo na tegemeo kubwa kwa wananchi wa maeneo mbalimbali mkoani Kilimanjaro¹²². Ukataji ovyo wa miti pia uliripotiwa katika maeneo ya wilaya ya Arumeru hasa katika msitu maarufu wa Meru. Msitu huo kwa muda mrefu sasa umevamiwa na watu wanaovuna miti pasipo kupanda mingine na kuitunza. Ukataji huu umekuwa kero kwa wananchi wengi wanaotegemea msitu huo kwa kupata maji kwa matumizi mbalimbali¹²³.

Habari nyingine za ukataji miti na uharibifu wa vyanzo vya maji ziliripotiwa katika maeneo ya wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara katika kijiji cha Loiborsitet.¹²⁴ Pia katika Mkoa wa Singida baadhi ya wananchi walivamia maeneo ya misitu ya Sekenke-Tulya, Minyughe, Mgori na Kisaki¹²⁵.

Ni dhahiri kuwa tishio la mabadiliko ya tabia ya nchi sio jambo la kujificha tena kutokana na kuwa dunia nzima sasa inapambana katika kuhakikisha kuwa kuna kuwepo na

¹²⁰ Nipashe Julai 25, 2011

¹²¹ Majira Aprili 5, 2011

¹²² Majira Septemba 17, 2011

¹²³ The Guardian Septemba 2, 2011

¹²⁴ Mwananchi Januari 15, 2011

¹²⁵ Nipashe Januari 15, 2011

jitihada za makusudi za kutokomeza visababishi vya mabadiliko haya. Ni wakati kwa serikali ya Tanzania na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na asasi za Kiraia kuhamasisha matumizi bora ya rasilimali na utunzaji wa mazingira ikiwa ni pamoja na misitu na vyanzo vya maji. Utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti pamoja na kuhakikisha kuwa viwanda vinatunza kemikali ambazo zinaweza kuathiri maisha ya binadamu, viumbe wengine na mazingira.

IX. UPIMAJI NA UMILIKI WA ARDHI

Masuala mengi yanayoibuka katika ardhi nchini yanasababishwa na ukosefu madhubuti wa upimaji wa ardhi kwa watumiaji mbalimbali. Kwa maeneo ya mijini kukosekana kwa upimaji wa viwanja kumepelekea kiwanja kimoja kuuzwa kwa zaidi ya mmiliki mmoja. Halikadhalika maeneo ya vijijini kutekelezwa kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kiwango kidogo umekuwa chachu ya kuibuka kwa migogoro ya ardhi baina ya makundi mbalimbali ya watumiaji hasa hasa wakulima na wafugaji pamoja na wanavijiji na wawekezaji. Kwa mwaka 2011 habari mbalimbali kuhusiana na masuala ya upimaji na umiliki wa ardhi ziliripotiwa kama ifuatavyo.

Wakazi wa Manispaa ya Moshi kata ya Longuo walipinga ubadilishaji wa matumizi ya ardhi kwajili ya ujenzi wa kiwanda karibu na makazi ya wananchi. Wananchi hao wanalalamika kuwa hofu yao kubwa ni uharibifu wa mazingira kwa njia mbalimbali¹²⁶.

Wilaya ya Rufiji ilitumia jumla ya Tsh. Milioni 250/- katika kutekeleza mpango bora wa matumizi ya ardhi kwenye vijiji 25 kwa matumizi ya Tsh. Milioni 10 kwa kila kijiji¹²⁷. Na huko Moshi katika kijiji cha Kindi, tarafa ya Kibosho Mpango wa Kurasimisha Mali za Wanyonge nchini (MKURABITA) uliwezesha kutoa hatimiliki za kimila kwa wanavijiji 4,500¹²⁸. Wakati huo huo serikali ilizitaka Halmashauri za majiji, miji na wilaya kuchangia gharama za kupima ardhi na kuwamilikisha wananchi ili waweze kushiriki katika kutekeleza kauli mbiu ya Kilimo Kwanza na mipango mingine ya maendeleo. Serikali ilizikumbusha halmashauri hizi kuzuia ujenzi holela, kupima viwanja na kutoa leseni za makazi au hatimiliki ni jukumu lao¹²⁹. Rai hiyo pia ilitolewa na Mbunge wa Ukerewe Mhe. Salvatory Macheleli¹³⁰.

Katika hali inayoonyesha kuwa wananchi wanatambua umuhimu wa ardhi yao kupimwa, huko Lushoto kwenye kata ya Tamota Kamati ya Maendeleo (WDC) iliomba

¹²⁶ Majira Julai 30, 2011

¹²⁷ Daily News Julai 27, 2011

¹²⁸ Nipashe Januari 15, 2011

¹²⁹ Nipashe Julai 29, 2011

¹³⁰ Majira Septemba 6, 2011

Halmashauri ya wilaya hiyo kuharakisha upimaji wa mashamba ya wananchi ili waweze kufaidika na mikopo mbalimbali¹³¹. Vile vile wakazi wa kata ya Maili Moja waliuomba uongozi wa Halmashauri ya wilaya ya Kibaha kuharakisha zoezi la upimaji ardhi wanazomiliki ili kutambulika kisheria jambo ambalo litawapa fursa ya kupata mikopo kwajili ya kuinua kipato chao¹³².

Wakati upimaji wa ardhi ukionekana kuwa ni suala nyeti katika wakati wa sasa hasa kutokana na kuongezeka kwa thamani ya ardhi duniani kote. Wizara ya Ardhi ilikiri kuwa kwa sasa Wizara ina wataalamu 450 tu kote nchini ambao ni sawa na asilimia 26 ya mahitaji ya wataalamu 1,400 wanaohitajika. Upungufu huu wa wataalamu unakwamisha shughuli nyingi ikiwa ni pamoja na upimaji wa ardhi kwenye maeneo mbalimbali nchini¹³³.

Habari njema katika eneo la upimaji wa ardhi lililoripotiwa kwa mwaka 2011 lilikuwa ni kwa serikali kupata vifaa maalum ambavyo vitapunguza gharama za upimaji kwa kiasi kikubwa. Kifaa hicho kinachoitwa Global Positioning System (GPS) kitakachokuwa kinatumia satelaiti¹³⁴.

X. MCHAKATO WA KATIBA MPYA NA NAFASI YA ARDHI

Tanzania inajiandaa na mabadiliko makubwa ya katiba ya nchi, mchakato wa kuwa na katiba mpya umeshaanza kwa hatua mbalimbali za awali. Katika mchakato huu kila kundi linashiriki kwa nafasi yake na kwa jinsi ambavyo lingetamani kuona yale wanayoyatetea yanafanyiwa kazi katika katiba mpya. Wanaharakati wa masuala ya ardhi nao ni sehemu ya makundi haya na madai makubwa ni kutaka kuona kuwa ardhi kama rasilimali muhimu kwa wananchi na Taifa inapata nafasi ya kutosha kwenye katiba mpya. Kwa maana hiyo masuala mbalimbali katika eneo hili yaliripotiwa kwa mwaka 2011.

Wanaharakati walitaka wananchi wote kwa pamoja na viongozi kuhakikisha kuwa kunakuwepo na ushiriki wa kutosha kutoka kwa makundi yote ili kuruhusu masuala yanayowagusa wananchi kama vile ardhi, ajira na maisha endelevu yanaingizwa kwenye katiba mpya¹³⁵. Pia iliripotiwa kuwa wananchi wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanakuwa mstari wa mbele wa kupata fursa ya kujadili hatima ya maisha yao kwa

¹³¹ Mwananchi Aprili 1, 2011

¹³² Machi 3, 2011

¹³³ Tanzania Daima Julai 29, 2011

¹³⁴ Mwananchi Agosti 2, 2011

¹³⁵ Mwananchi Septemba 21, 2011

rasilimali zote kusimamiwa kikatiba. Hii ni kutokana ukweli kuwa maendeleo ya nchi na wananchi yanategemea rasilimali zenye usimamizi dhabiti¹³⁶.

XI. SUALA LA ARDHI KATIKA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

Ni muda mrefu sasa kumekuwa na mazungumzo na mijadala ya hapa na pale kuhusiana na suala la matumizi na umiliki wa ardhi katika nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mwaka 2011 mwezi wa Julai Katibu wa Jumuiya hiyo Dk. Richard Sezibera alinukuliwa akisema kuwa suala la umiliki wa ardhi litaendelea kuwa ndani ya mamlaka ya nchi husika katika hatua yoyote itakayofikiwa katika ushirikiano huo. Lakini katika hali ya kushangaza mwisho mwa mwaka 2011 iliripotiwa tena kuwa makubaliano ya kusaini mkataba wa ushirikiano wa maeneo mbalimbali yalikuwama kutokana na Tanzania kugoma kusaini kutokana na kipengele kilichoonyesha kuwa ardhi ya nchi zote za Jumuiya itatumika kwa pamoja, jambo ambalo Tanzania haikukubaliana nalo.

Ni ukweli ulio wazi kuwa Tanzania inahitaji mijadala mkubwa na wa muda mrefu kuhusu rasilimali zake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hii ni kutokana na kuwa suala la kuahirisha kusaini makubaliano ni suala la muda tu ambalo mwisho wa siku ni lazima makubaliano yasainiwe. Kwa maana hiyo serikali na wananchi waone umuhimu wa kujadili suala hili kwa mapana na marefu.

XII. MRADI WA MJI MPYA KIGAMBONI

Serikali chini ya usimamizi wa Wizara ya Ardhi na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ipo katika mchakato wa mradi wa ujenzi wa mji mpya wenye hadhi ya kimataifa katika eneo la Kigamboni. Mchakato wa ujenzi wa mji huu ambao ulianza mapema mwaka 2008 umezua taharuki miongoni mwa wakazi wanaoishi katika eneo hili ambao wengi wao wamekuwa wakilalamika kuwa hawatambui hatima ya maisha yao itakuwaje kutokana ujenzi huo. Kwa mwaka 2011 habari mbalimbali kuhusiana na mradi huu ziliripotiwa kama ifuatavyo.

Wakazi wa Kigamboni waliishutumu Wizara ya Ardhi kwa kuchukua maeneo yao pasipo kuwashirikisha. Wakazi hao walilalamika kuwa taratibu zilizoendelea kwenye eneo la mradi wa ujenzi wa mji mpya ni sawa na kuwadhulumu wanyonge haki zao. *“Wizara haikutuhusisha katika hatua za awali za mradi huu wala ramani yake hatukuifhamu, tunapohoji tunambiwa Mbunge na Diwani wetu watajulishwa”* walisema wakazi hao wa Kigamboni¹³⁷. Halikadhalika wakazi wa Kigamboni walilalamikia suala la utambuzi wa

¹³⁶ Nipashe Agosti 31, 2011

¹³⁷ Tanzania Daima Februari 10, 2011

nyumba za wakazi wa eneo hilo kwa madai kuwa liligubikwa na utata mkubwa kutokana na Wizara ya Ardhi kutoa majina ya watu ambao hawajawahi kuwa wakazi wa maeneo hayo kabla ya kutambulishwa mradi wa mji mpya. Wakazi hao walilalamika kuwa zoezi la utambuzi wa nyumba liliendeshwa katika hali ambayo haikuwa wazi na shirikishi jambo ambalo linatia shaka haki stahiki kwa wakazi halali¹³⁸. Katika hali iliyoonyesha kupotea kwa imani ya wakazi wa Kigamboni kwa serikali, Mbunge wa Kigamboni Dk. Faustine Ndugulile aliwajia juu baadhi ya watendaji wa Wizara ya Ardhi ambao walionekana kuwa waroho kwa kutaka kujitajirisha wao wenyewe kupitia mradi wa ujenzi wa mji mpya. Mbunge huyo aliyasema hayo baada ya malalamiko kutoka kwa wananchi wa Kigamboni kuwa kuna majina ya bandia katika orodha ya utambuzi wa nyumba za eneo la mradi¹³⁹.

XIII. UWEKEZAJI KATIKA ARDHI YA VIJJI KWA UZALISHAJI WA NISHATI UOTO

Uwekezaji katika ardhi ya vijiji kwajili ya nishati uoto ni uwekezaji ambao ulianza mapema miaka ya 2000 katika hatua za awali za wawekezaji kupata mashamba ya kulima mazao tofauti tofauti kwajili ya kilimo hicho. Mchakato huo ulichukua sura tofauti tofauti ikiwa ni pamoja na kupingwa na wanaharakati mbalimbali wa masuala ya ardhi na mazingira. Pamoja na jitihada hizo za wanaharakati bado makampuni mbalimbali ya kigeni yalifanikiwa kupata mashamba maeneo mbalimbali nchini kwa kilimo hicho kama vile maeneo ya wilaya za Kilwa, Kisarawe, Rufiji, Bagamoyo, mkoa ya Kigoma, Rukwa, Arusha na kwingineko.

Baada ya muda wa takribani nusu muongo matokeo ya uwekezaji huu yameanza kuonekana katika baadhi ya maeneo ambako makampuni mbalimbali yaliwekeza. Matokeo haya ni pamoja na makampuni hayo kushindwa kuendeleza na uzalishaji katika mashamba waliyochukua; wawekezaji kushindwa kutekeleza ahadi walizoahidi kwa wanavijiji wakati wanachukua mashamba yao; pamoja na wanavijiji kutolipwa fidia za mashamba na mazao yao yaliyochukuliwa.

Kutokana na matokeo haya yote jambo kubwa lililoonekana kwa mwaka 2011 ni kuwa mchakato mzima wa uwekezaji katika ardhi ya vijiji kwajili ya nishati uoto ulikosa ushirikishwaji wa wanavijiji na viongozi wao. Utwaaji wa mashamba ya vijiji kwa wawekezaji aidha yalifanyika kwa mbinu ya baadhi ya watendaji wa Halmashauri za

¹³⁸ Nipashe Agosti 1, 2011

¹³⁹ Nipashe Agosti 3, 2011

wilaya au yalifanyika kwa ushawishi wa viongozi wa ngazi za juu kwa ahadi kwa wananchi kuwa uwekezaji huo utaondoa umaskini na kuboresha maisha yao¹⁴⁰.

3. HITIMISHO

Tathmini ya jumla inaonyesha kuwa masuala ya ardhi yaliripotiwa zaidi kwa mwaka 2011 baada ya masuala ya siasa na uchumi. Jambo kubwa lililojitokeza katika kuripotiwa huku kwa masuala ya ardhi ni kuwa mengi ya masuala haya yalikuwa yamejikita zaidi katika matatizo yanayoikumba sekta ya ardhi kuliko mafanikio katika sekta hii. Hali hii inadhihirishwa na idadi kubwa ya migogoro ya ardhi iliyoripotiwa baina ya makundi mbalimbali ya watumiaji wa ardhi. Pia masuala ya uvamizi wa maeneo na ulipwaji wa fidia usioridhisha wananchi hali iliyopelekea malalamiko mengi. Kwa maana hiyo ni jukumu la serikali, wadau mbalimbali kama vile asasi za kiraia pamoja na wananchi wenyewe kuitazama ardhi kama rasilimali muhimu inayohitaji kutazamwa kwa umakini zaidi ili nchi isije kutumbukia katika migogoro ya mara kwa mara inayosabishwa na mgawanyo mbovu wa rasilimali miongoni mwa wananchi.

¹⁴⁰ Daily News Aprili 2, 2011